# Nipashe

Alhamisi Oktoba 15, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580369

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**MDEE** atangaza kukata rufani kupinga adhabu kusimamisha kampeni UKURASA 3



**MGOMBEA** CHAUMMA amtaja Maalim Seif urais wa Zanzibar UKURASA 3

**Neymar asifiwa kuvunja rekodi ya Ronaldo Brazil** UKURASA 22

# VILIO DAR

• **Mvua** yasababisha vifo vya watu 8, watano familia moja wafa kwa moto, mahabusu auawa kwa radi, JPM aahidi bil. 32/- kukabili mafuriko... *Endelea uk.2,4*

## Lissu kuunda tume kero za uvuvi

UKURASA 3



Mkuu wa Wilaya ya Arusha Mjini, Kenan Kihongosi (aliyeshika bendera), akiongoza matembezi ya pamoja na wakazi wa jijini Arusha jana, kwa ajili ya kumbukizi ya miaka 21 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



## Magufuli aahidi kuendeleza mambo aliyoyaacha Nyerere

UKURASA 2










Mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli, akisalimia baada ya kuwasili katika viwanja vya Tanganyika Packers, eneo la Kawe, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya mkutano wa kampeni. Kulia ni Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally. **PICHA: IKULU**

# Magufuli aahidi kuendeleza mambo aliyoyaacha Nyerere

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amesema mwasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, amwaachia Watanzania mambo makubwa matano ambayo ameahidi kuyasimamia na kuyaendeleza.

Sambamba na hayo, amesema Mwalimu Nyerere alikuwa mtu wa kipekee barani Afrika na duniani kwa kuwa alikuwa shupavu, jasiri, mwenye maono, mwanamapinduzi, mpenda amani na mshikamano, na mtu mwenye ushawishi.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana katika Viwanja vya Tanganyika Packers, Kawe jijini Dar es Salaam wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, akiwaomba kura Watanzania na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliojitokeza kumsikiliza.

"Mwalimu Nyerere kuzaliwa Tanzania tunapaswa kumshukuru Mungu. Alikuwa mtu wa pekee, si kwa Tanzania tu bali Afrika na dunia kwa ujumla. Alikuwa mtetezi wa wanyonge na amepigania ukombozi wa nchi nyingi barani Afrika," alisema.

Mwalimu Nyerere ambaye aliongoza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na baadaye kuanzishwa kwa taifa la Tanzania kwa kuunganishwa Tanganyika na Zanzibar, jana ilikuwa kumbukizi ya miaka 21 tangu alipofariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, London, Uingereza, alikokuwa akipatiwa matibabu.

**MAMBO ALIYOYAACHA**

Rais Magufuli alisema Mwalimu Nyerere amewaachia Watanzania mambo makubwa matano ambayo yanapaswa kuenziwa, huku naye akiahidi kuyaenzi na kuyaendeleza.

Jambo la kwanza, kwa mujibu wa Rais Magufuli, uhuru wa nchi. Alisema Mwalimu Nyerere aliongoza harakati za ukombozi ambazo alianzia katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kushirikiana na wazee wa kilichokuwa chama cha ukombozi cha TANU.

"Mwaka 1961 Mwalimu Nyerere alisema uhuru tulioupata ulikuwa uhuru wa kweli. Hata marais waliomfuata walijitahidi kuendeleza na kuenzi uhuru wa nchi yetu, hata mimi nitaendelea kuenzi," alisema.

Katika kuhakikisha uhuru huo unakuwa wa kweli, Rais Magufuli alisema Nyerere alikuwa tayari kuvunja uhusiano na mataifa yaliyokuwa na nguvu ya kiuchumi na kijeshi.

"Hata wakati wa janga la corona, tulipewa masharti kufunga mipaka yetu, lakini tulimtanguliza Mungu. Tulifanya hivyo kwa kuzingatia misingi ya Mwalimu Nyerere na wako waliotupinga na walitutangaza vibaya kimataifa. Hata wakati wa Bunge la Bajeti walitoka nje na sasa wako kwenye kampeni. Hao ni vibaraka tunapaswa kuwakataa," alisema.

Rais Magufuli alisema jambo la pili ni amani na utulivu kwamba Mwalimu Nyerere alipenda amani ndani na nje ya mipaka ya Tanzania huku akitolea mfano kwamba wakati anafariki dunia, alikuwa mpatanishi wa mgogoro wa Burundi.

"Kamwe Watanzania tusikubali kufarakanishwa. Ikivunjika amani hatutaweza kukimbia, watoto, kinamama na wazee ndio watakaoathirika. Amani ndiyo uchumi wa nchi yetu," alisisitiza.

Rais Magufuli alisema jambo la tatu ni umoja na mshikamano. Alisema Mwalimu Nyerere aliyaunganisha zaidi ya makabila 120 kwa lugha ya Kiswahili na kuwa wamoja.

Wakati Mwalimu alifanya hivyo, alisema kuna baadhi ya nchi zina makabila mawili, au matatu lakini zimeshindwa kuungana na kuwa taifa moja, lakini kuwa na umoja.

"Hapa kwetu ukienda Mbeya utakuta Wachaga wanaishi na kufanya shughuli zao bila kubaguliwa, Kagera wako Wasambaa, Mwanza kuna Wamasai wanaishi bila ya kubaguliwa, Zanzibar kuna Wamasai, Pemba kuna Wakurya.

"Hata Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam siyo Mzaramo. Nenda Lindi, Ruvuma, Morogoro wakuu wa mikoa si watu wa kule, wanatoka sehemu zingine. Yote hayo yamewezekana kwa sababu ya Nyerere," alisema.

Rais Magufuli alisema jambo la nne ni Muungano akibainisha kwamba Mwalimu Nyerere amewaachia Watanzania Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ulizaa taifa la Tanzania.

Alisema Muungano huo ulitokana na uhusiano wa kihistoria baina ya watu wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na maono ya waasisi wake, Mwalimu Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume (naye sasa ni marehemu).

"Tunataka viongozi wa kuendelea kuuenzi Muungano. Ukienda Namanga (Dar es Salaam) kuna Wapemba wana maduka yao, Lindi kuna Wanyakyusa. Muungano unajenga undugu na ujamaa. Mkinichagua nitaendelea kuuenzi na kuulinda Muungano na Dk. Hussein Ali Mwinyi (mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM),"alisema.

Alilitaja jambo la tano kuwa ni ujenzi wa uchumi wa nchi kwa kutumia rasilimali zake. Katika hilo, alisema Nyerere alisisitiza kujenga uchumi wa nchi na kuwa taifa linalojitegemea.

"Hatuna budi kuendelea kutumia rasilimali tulizo nazo. Mwalimu Nyerere alihimiza kutumia juhudi zetu na rasilimali tulizo nazo. Pia alisisitiza watu kufanya kazi kwa bidii na hiyo ninaienzi ndiyo maana kaulimbiu yangu ni 'Hapa Kazi Tu'.

Hata katika nukuu zake aliwahi kusema serikali isiyokusanya kodi ni serikali ya wala rushwa," alisema.

Katika kuhakikisha hayo yanatimia, alisema Mwalimu Nyerere alianzisha mashirika mbalimbali kama vile Shirika la Ndege Tanzania (ATC sasa ATCL), Shirika la Reli Tanzania (TRC), Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

"Wakati anaanzisha mashirika hayo alipata upinzani mkubwa. Nawahakikishia Watanzania serikali ya awamu ya tano itajitahidi kuwa na maono ya Baba wa Taifa," alisema.

# Mvua yaacha vilio jijini Dar

**Na Romana Mallya**

WATU 13 wamefariki dunia, wakiwamo wanane ambao vifo vyao vimetokana na mvua kubwa iliyonyesha juzi jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, watu watano ambao ni wa familia moja wamefariki dunia baada ya nyumba waliyokuwa wakiishi kuungua moto.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala, Janet Magomi, alisema vifo vilivyotokana na mvua vimetokea Mto Msimbazi.

Alisema kwamba, Mto Msimbazi eneo la Kariakoo kulikutwa miili ya watu watano ambayo imehifadhiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kati yake, mitatu tayari imeshatambuliwa na ndugu zao.

"Maeneo ya Buguruni, kuna taarifa ya watu wengine wawili, mwanaume na mwanamke ambao miili yao iliokotwa kwenye mto na maeneo ya Ukonga ipo taarifa ya mtu mmoja aliyeokotwa Mto Mvule, miili yote ipo Muhimbili," alisema.

Kamanda Magomi alisema kati ya watu hao waliofariki dunia kutokana na mvua hizo za juzi, watoto ni wawili.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, watoto hao walifariki dunia wakati wakisaidiana kuokoana kwenye Mto Msimbazi.

Kuhusu tukio la moto, Kamanda Magomi alisema lilitokea juzi saa nne usiku Kata ya Pugu, Tarafa ya Ukonga wilayani Ilala jijini.

"Kuna nyumba iliungua na wamefariki wanafamilia watano ambao ni mke, watoto watatu na wifi ambaye ni mdogo wa mume wa mke aliyefariki dunia," alisema.

Kamanda Magomi alisema watu hao walifariki dunia baada ya kufikishwa hospitalini.

"Walikuwa hawana majeraha wakati wakipelekwa hospitali, lakini wakati wakitaka kupatiwa matibabu, walionekana wameshafariki dunia, chanzo cha moto huu tunaendelea kuchunguza ila mashuhuda wanasema ulianzia sebuleni," alisema.

Aliongeza kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilifika eneo hilo la tukio na kuuzima ili usiendelee kuleta madhara zaidi.

**HABARI KITAIFA**

# Mgombea urais wa CHAUMMA amtaka Maalim

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia tiketi ya Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Ali Omar Juma, amesema yeye na chama chake wamekubaliana kumuunga mkono mgombea wa nafasi hiyo kupitia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kile alichoeleza kuwa ana kila sifa ya kuwa Rais wa Zanzibar.

Juma aliyasema hayo kisiwani Pemba katika Viwanja vya Ditia Jimbo la Wawi Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini katika mkutano wa kampeni uliondaliwa na ACT-Wazalendo kupitia mgombea wao wa urais.

Kupitia mkutano huo Juma aliwataka wanachama wote kumpigia kura Maalim Seif ili awe Rais kwa madhumuni ya kuikomboa Zanzibar.

"Sisi sio wanafiki, lazima tumuunge mkono Maalim Seif kwa sababu hajawahi kushindwa na CCM, na lengo lake ni kuikomboa Zanzibar. Kwa nini. CHAUMMA isimuunge mkono Maalim? Alihoji Juma.

Alisema kilichowashawishi ni nia njema aliyonayo Maalim Seif ya kudai Zanzibar yenye mamlaka kamili.

"Sisi tukiwa na mamlaka yetu ina maana ajira zitaongezeka kupitia taasisi mbalimbali ambazo zitaanzishwa Zanzibar kupitia Umoja wa Mataifa pamoja na taifa moja moja," alisema Juma. Naye Maalim Seif katika mkutano alizungumzia hali ya watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kudai kuwa wana hali ngumu ya maisha.

Alisema akiingia madarakani atahakikisha atarejesha posho zote ambazo waliokuwa watumishi wa umma wakinyimwa katika serikali zilizopita na kueleza ni haki yao halali.

Alisema mara nyingi wanaopewa posho ni viongozi wakubwa tu na huku wafanyakazi wa chini wakiachwa bila kulipwa posho wanazostahili. Maalim Seif aliwatambulisha kwa wananchi wagombea ubunge, uwakilishi na udiwani katika Jimbo la Chakechake na Wawi katika Wilaya ya Chakechake.

# Lissu aahidi kuunda tume ya kuchunguza kero za wavuvi

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais (CHADEMA) Tundu Lissi, jana alilazimika kutumia usafiri wa boti kwenda visiwa vya Ukerewe kuwafikia wapigakura baada ya kukosa kivuko ambacho ilidaiwa kiko kwenye matengenezo.

Katika kampeni zake, Lissu alisema akiingia madarakani, jambo la kwanza ataunda Tume ya Majaji wa Mahakama za Juu kuchunguza matukio yote ya kuumiza watu, kuteka watu, kutia umaskini ambayo yamefanyika kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, ili kufahamu nani aliamuru hayo kutokea, aliyetekeleza na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Hakuna sheria ya nchi inayosema ukikuta mtu Ziwa Tanganyia au Victoria adhabu yake kifo, mimi sijaona sheria ya namna hiyo, tutachunguza matukio yote ya mauaji ili tufahamu nani aliyeamuru, aliyetekeleza na nani ashughulikiwe," alisema.

"Kwa sababu kuua ni kosa, lazima wote walioathirika waliouliwa ndugu zao wafidiwe, walioumizwa wafidiwe, waliotiwa umaskini wafidiwe," alisema.

Alisema jambo la pili litakalofanywa ni kubadili sheria na kanuni za uvuvi ili kuhakikisha mambo mabaya hayatokei kwa makundi hayo.

Lissu alisema jingine atakaloshughulikia ni miundombinu karibu na Kisorya ambako kuna umbali mdogo na Kisiwa cha Ukerewe chenye watu zaidi ya 300,000, akiahidi atajenga daraja ili wapate usafiri wa uhakika.

Alisema alilazimika kutumia usafiri wa boti baada ya mara kadhaa kuambia kivuko hicho ni kibovu jambo ambalo kwake aliona ni mbinu kumzuia kuwafikia wananchi wa eneo hilo.

Akizungumza akiwa ndani ya boti hiyo, Lissu alisema zaidi ya mara mbili amefika eneo la Kisorya ili kuvuka lakini alishindwa kwa sababu zilizotolewa na wasimamizi wa kivuko hicho.

"Nimepanda boti baada ya kukosa Kivuko cha kupanda, nilikuja wiki mbili zilizopita kwa ajili ya kampeni, lakini nilishindwa kupanda, yote hii ni kutuzuia tusivuke, lakini tumetumia usafiri mwingine na tumevuka salama, haya yote tumeona ni namna ya kutuzuia kupanda usafiri huo kuwafikia wananchi wa Ukerewe kwa ajili ya kuwafikishia taarifa.

"Kwetu ni Singida, hatuna ziwa, sijawahi kuogelea, lakini nikawaambia watu wangu kama ni kuogelea nitajifunza leo, lakini niende Ukerewe nikazungumze na wana Ukerewe, ninasikia polisi walitaka kuzuia huu mkutano, hawaruhusiwi kuzuia zaidi ya kulinda usalama. Nilisema hata wanizuie lazima nije hapa.

"Poleni sana kwa haya, msivunjike moyo yana mwisho haya na mwisho wake ni Oktoba 28 mwaka huu. Ninawashukuru kwa kuwa sehemu ya kitovu cha mabadiliko ya nchi hasa Kanda ya Ziwa," alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, namna ya kumwenzi Baba wa Taifa siyo kuruhusu wanaomheshimu kutoa heshima alikolala, bali kuyaishi mawazo na fikra zake ambazo wengi wameshindwa kuyaenzi. Mgombea huyo alisema Ilani ya CHADEMA inazungumzia uhuru, haki na maendeleo ya watu na kwamba mwaka 1968 aliandika kitabu na kukiita 'Uhuru na Maendeleo', ambacho alisema maendeleo maana yake ni maendeleo ya watu na siyo vitu. Alisema wananchi wa kisiwa na maeneo hayo ni wavuvi, lakini hali zao ni mbaya kwa kuwa kuna waliopoteza maisha, kuchomewa nyavu na mitumbwi na wengine wameishia kwenye umaskini mkubwa. "Ninasema mkinichagua Oktoba 28 mwaka huu, haya mambo ya kunyanyasa wavuvi, kuwatia umaskini itakuwa ni mwisho," aliahidi.



Wakazi wa Kata ya Saranga, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, wakivuka kwa foleni kupitia sehemu ndogo ya daraja lijulikanalo kwa jina la Super Star, ambalo limevunjika kutokana na mvua kubwa iliyonyesha juzi, na kusababisha magari na vyombo vingine vya usafiri kushindwa kupita. **PICHA: BEATRICE MOSES/TUDARCo**

# Mdee atangaza kukata rufani kupinga kusimamisha kampeni

**Na Christina Mwakangale**

MGOMBEA ubunge wa Kawe (CHADEMA), Halima Mdee, amesema atakata rufani kupinga uamuzi uliotolewa na msimamizi wa uchaguzi, kumsimamisha kufanya kampeni kwa siku saba.

Mdee ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake la chama hicho (BAWACHA), alitangaza kusudio lake hilo jijini Dar es Salaam juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu suala hilo.

"Sijakubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi Kinondoni kunisimamisha kufanya kampeni kwa siku saba, nitakwenda tume kupeleka rufani yangu, kamati imetoa hukumu bila kunisikiliza," alisema.

Mdee ambaye amekuwa Mbunge wa Kawe kwa miaka 10 mfululizo, alisema tuhuma zilizosababisha akumbane na adhabu hiyo ni kumchonganisha Askofu Josephat Gwajima na madhehebu mengine na waumini wake. Gwajima anawania ubunge wa jimbo hilo kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Nipashe ilimtafuta Msimamizi wa Uchaguzi Kinondoni, Aron Kagurumjuli, kuzungumzia suala hilo, lakini simu yake ilikuwa inaita bila kupokewa.

"Siongei haya ili kutaka huruma na ninaelewa mnanifahamu, sijazoea huruma mimi wala kubebwa, hizo siku saba hata wangesema wanipe miezi miwili Gwajima nishamgalagaza na analijua hilo.

"Ushahidi uliopelekwa dhidi yangu, uko nje ya matakwa ya sheria, sikufanya kampeni eneo husika wala tarehe iliyotajwa," Mdee alidai. Kada huyo wa CHADEMA alibainisha kuwa, tangu Oktoba 11 mwaka huu, alizuiwa kufanya kampeni kwa siku saba kutokana na kile alichoambiwa ni ukiukaji wa maadili. Mdee amekuwa sehemu ya wagombea ubunge kupitia CHADEMA waliozuiwa kufanya kampeni kwa siku kadhaa hivi karibuni, wakiwamo Boniface Jacob (Ubungo, siku saba) na Gerva Mgonja (Same Magharibi, siku 14), huku Salome Makamba akipewa onyo kutokana na kudaiwa kukiuka maadili kwenye kampeni za ubunge wa Shinyanga Mjini.

IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY IN HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA
LAND APPEAL NO. 31/2020
(Arising from Land Application no. 182/2015 Bukoba District Land and Housing Tribunal)
IDIASA AMRI SALIMU ....................................APPELLANT
VERSUS
1. SAIDA AMANYA SAID
2. MUJIBU RUBAGUMYA ADAMU ...............RESPONDENTS
TO, MUJIBU RUBAGUMYA ADAMU
RE: NOTICE FOR DATE OF MENTION

Whereas the above mentioned Appellant has lodged a case registered as land appeal no. 31/2020 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 3rd day of November, 2020 at 09:00 am before Hon. Judge F.H. Mtulya.
You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Give under my hand and seal of the court this 12th day of October,2020.

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
BUKOBA.

# JPM aahidi kumaliza mafuriko Dar

**Na Gwamaka Alipipi**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, amesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, atahakikisha anamaliza tatizo la mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam.

Amesema mojawapo ya mikakati iliyowekwa ni kutengwa Sh. bilioni 32 kwa ajili ya kuukarabati Mto Ng'ombe, ambao umekuwa ni kero na chanzo cha mafuriko nyakati za mvua.

Alitoa ahadi hiyo jana kwenye viwanja vya Tanganyika Parkers wakati wa kampeni, akiwahutubia wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza kumsikiliza.

"Endapo mkinichagua, nitahakikisha kero ya mvua ya maji kujaa tunaitatua. Tumetenga Sh. bilioni 32 kwa ajili ya kuukarabati Mto Ng'ombe. Suala lote la mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam, tunakwenda kulimaliza," alisema Dk. Magufuli.

Hata hivyo, alieleza kuwa kuna baadhi ya wananchi wamekuwa chanzo cha mafuriko kwa kujenga ukuta kandokando ya mito, kuziba mitaro ya kupitishia maji.

Alisema: "Unajenga nyumba kwenye mto, unajenga ukuta kwenye ukingo wa mto unatarajia maji yapite wapi? Lazima yatapita kwenye makazi ya watu."

Kadhalika, Rais Magufuli alisema serikali imejitahidi katika kuleta mafanikio nchini ikiwamo ukusanyaji wa mapato kwa wingi.

Alisema mapato ya kodi yameongezeka kutoka Sh. bilioni 800 hadi Sh. trilioni 1.5, makusanyo katika halmashauri nayo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 379 hadi Sh. bilioni 713.5, gawio la serikali kutoa Sh. bilioni 161 hadi Sh. trilioni 1.05.

**AMNADI GWAJIMA**

Wakati huohuo, Dk. Magufuli aliwataka wananchi wa Jimbo la Kawe kuhakikisha wanamchagua Askofu Mkuu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, kuwa mbunge wao.

Alisema: "Wananchi wa Kawe hamjamkosea Mungu, nileteeni Gwajima alete maendeleo ya kweli, kwenye kura za maoni hakuongoza, aliyeongoza ni mtoto wa dada yangu anaitwa Furaha, wa pili alikuwa Angellah Kiziga, lakini hao wote hawana uwezo kama Gwajima."

Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Dk. Bashiru Ally, alisema chama hicho kimemaliza awamu ya tano ya kampeni katika Jiji la Dar es Salaam na kinakwenda kuzindua awamu ya sita, ambayo itakuwa ni ya lala salama.

Hivyo, aliwataka wanachama wa chama hicho kujielekeza katika mafunzo ya namna ya kupiga kura, pamoja na kuwa na moyo wa uvumilivu. Alisema Jiji la Dar es Salaam ni kitovu cha harakati za ukombozi kwa baadhi ya nchi za Afrika, litaendelea kuwa kitovu cha ukombozi na kiuchumi.

Alieleza kuwa walipa kodi, wapigakura wengi wapo katika Jiji hilo na kwamba kwa maendeleo ya kisasa Jiji la Dar es Salaam linaongoza.



Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Msafiri Mbibo (kulia), akizungumza na Katibu Tawala wa Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, Sarah Komba, alipomtembelea ofisini kwake, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Radi yaua mahabusu, wanne wajeruhiwa

**Na Futuna Seleman,** KIBITI

MAHABUSU Mussa Hajji Mshana (25), aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya mauaji, amefariki dunia katika Gereza la Wilaya la Mng'alu Kibiti baada ya kupigwa na radi, huku wengine wanne wakijeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Onesmo Lyanga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi majira ya saa sita mchana katika gereza hilo.

Aliwataja waliojeruhiwa ni mfungwa Richard Mai (24) mfungwa namba 37/2020, Hashim Rashid (26) namba 154/2020, Ismail Mtupa namba 155/2020 na Issa Hajji (21) namba 31/2020, ambao wanaendelea na matibabu katika Kituo cha Afya Ikwiriri. Alitoa wito kwa wananchi kanda maalum ya Kibiti, Rufiji, Mafia na Mkuranga kuchukua tahadhari wakati wa kipindi chote cha mvua za vuli zinazoendelea kunyesha nchini.

"Ni vyema wananchi wachukue tahadhari kipindi hiki cha mvua matukio mengi yanaweza kujitokeza wanoishi mabondeni nao wahame mara moja ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea wananchi mashambani wachukue tahadhari hasa msimu huu mvua zinaendelea kunyesha," alisema kamanda Lyanga.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, hakuna mahabusu wala mfungwa aliyekimbia kufuatia tukio hilo, na kwamba ulinzi na usalama vimeimarishwa kanda yote ya mkoa wa kipolisi Rufiji.

## Serikali yaagiza kununuliwa ndege kukabili majanga

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, ameagiza Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), kujipanga upya kwa kuwa na utayari wa kukabiliana na majanga ya moto yanapotokea katika maeneo ya hifadhi nchini.

Ametaka shirika hilo kwa kushirikiana na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), kununua helikopta yao maalum itakayokuwa ikitumika kukabiliana na majanga ya moto kisayansi zaidi.

Maelekezo mengine aliyoyatoa baada ya kupokea taarifa kuhusu tathmini ya udhibiti wa moto uliozuka katika Mlima Kilimanjaro Oktoba 11 mwaka huu, ni pamoja na kuwekeza katika uboreshaji wa miundombinu ya kuzimia moto mlimani.

Akiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro jana, Dk. Kigwangalla alitembelea eneo lilioathiriwa na moto na kubainisha kuwa asilimia 1.6 ya hifadhi ya mlima huo ndiyo imeathirika na moto huo.

"Nimewaagiza TANAPA kuhakikisha wanawekeza katika miundombinu, maeneo yenye vifaa vidogo vya kuzimia moto, viwekwe vikubwa na vya kisasa vitakavyoweza kusaidia uzimaji wa moto kwa haraka zaidi.

"Pamoja na uwekezaji wa miundombinu, pia tunatarajia kununua helikopta maalumu itakayokuwa na vikapu maalum vya kuzima mara inapotokea majanga kama hayo," alisema.

Alisema matukio ya moto yamekuwa yakitokea kwenye mlima huo, lakini uzimaji moto umekuwa ukifanyika kwa kutumia zana za kizamani, hivyo kusababisha moto kuchukua muda mrefu na kuleta madhara makubwa.

Waziri huyo alisema moto huo umeathiri eneo la ukanda wa tatu kati ya kanda tano za mlima huo.

"Katika eneo lililokabiliwa na moto, ni eneo la vichaka vifupi, ambapo hukaa nyoka, mijusi na ndege, lakini shughuli zote za kiutalii zinaendelea, wanaopanda na kushuka wote wapo salama," alisema.

HABARI KITAIFA

# Watanzania watakiwa kumwenzi Nyerere kwa kudumisha amani

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kulinda amani, umoja na mshikamano vilivyopo ili waendelee kufanya shughuli zao kwa uhuru bila vurugu na kujiletea maendeleo, kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alisema hayo jana wakati akitoa salamu za taasisi hiyo kuhusu kumbukumbu ya miaka 21 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema kumbukumbu ya miaka 21 ya kifo cha Baba wa Taifa, imekuja wakati zimebakia wiki chache Watanzania washiriki katika uchaguzi mkuu. "Sisi kama watu tunaohimiza utawala bora, hatunabudi kuendelea kuwakumbusha Watanzania kulinda, amani umoja na mshikamano kwa ajili ya vizazi vilivyopo na vijavyo," alisema Ngawaiya. Alisema kuvunja amani ni rahisi, lakini kurudisha ni vigumu, hivyo ili kumuenzi Baba wa taifa, kila Mtanzania anatakiwa kuwa mtu wa kuhimiza mwenzake kulinda amani iliopo nchini. "Niwakumbushe tu kwamba, Baba wa Taifa alianza kazi ya kupigania amani na hata alipong'atuka aliendelea kuhimiza amani, hivyo amani iwe ni wimbo wa kila mmoja na hasa wanasiasa," alisema.

Alisema, wakati wa kampeni, wanasiasa wawe makini na kuepuka kutukana wenzao ama kutumia maneno ya kuudhi badala yake watangaze sera na ilani za vyama vyao kwa wananchi.

"Kama watu wanakupenda watakuchagua tu bila hata kutukana ama kutumia lugha ya kuudhi dhidi ya wagombea wengine, kwani kufanya hivyo kunaweza kuamsha hasira za watu na kusababisha amani ivurugike," alisema Ngawaiya.

Aliongeza kuwa, Watanzania ni watu wa amani, hivyo wasiingizwe katika mambo ambayo hawakuyazoea, na kwamba hawana ujasiri wa kupigana kama walivyo baadhi ya wengine ambao nchi zao hazina amani.

# Kukosekana wakalimani kwa wakwaza walemavu

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Wakalimani wa lugha ya alama nchini, kimeeleza kuwa uchache wa wakalimani kunasababisha wenye ulemavu husussan viziwi kukosa ujumbe kwenye mikutano ya kampeni.

Billbosco Muna, mwenyekiti wa chama hicho, alisema hakuna wakalimani katika mikutano ya kampeni inayoendelea nchini, hivyo ujumbe hauwafikii watu ambao ni viziwi.

Muna aliyasema hayo katika mahojiano na kituo kimoja cha redio akizungumzia umuhimu wa wakalimani wa lugha kwa kundi la wenye ulemavu.

"Kuna idadi ndogo ya walimu wenye ujuzi wa kukalimani lugha mbalimbali, ili kumfikia mwenye ulemavu ujumbe unaotolewa hasa mikutano ya kampeni.

Kuna baadhi ya vyombo vya habari hutumia wataalamu hawa," alisema Muna na kuongeza:

"Tunaposema ukalimani ni mchakato kutoka kwa mpokeaji yaani mkalimani aibadili lugha kwenye ubongo wake na kuufikisha ujumbe kwa lugha ya alama kwa kiziwi." Waziri Mkuu, Kassimu Mjalaiwa, Septemba mwaka jana, wakati akihutubia wananchi kwenye kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Viziwi Duniani, alisema mitaala ya vyuo vya afya, polisi, mahakama na vinginevyo vihakikishe vinaongeza kozi ya lugha ya alama.

Alisema lugha hiyo iwe kama somo, la lazima ili kusaidia kuzalisha watalaamu wa lugha ya alama ambao wataweza kuwahudumia viziwi ipasavyo.

"Utoaji wa elimu katika ngazi mbalimbali pamoja na kuboresha mawasiliano katika jamii na tayari imetoa mafunzo ya lugha hiyo awamu ya kwanza kwa walimu 82 wa shule za sekondari," alisema.

# Watumia kemikali wapatiwa elimu

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amewataka wajasiriamali wanaotumia kemikali katika uzalishaji wa bidhaa kuzingatia matumizi salama.

Dk. Mafumiko alitoa rai hiyo juzi wakati akifunga mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wanaotumia kemikali yaliyoandaliwa na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kupitia Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Ilala jijini Dar es Salaam.

"Kemikali ni hatari zisipotumiwa kwa uangalifu zinaweza kutumika kama silaha, kwa sababu mtu akimwagiwa usoni inaweza kusababisha upofu. Matumizi yakiwa mabaya yanaweza kuleta madhara kwa nchi kama ilivyotokea nchini Lebanon kwa kemikali kulipuka na kusababisha vifo na uharibifu wa mali," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Namba 3 ya Mwaka 2003, ofisi yake imepewa jukumu la kutoa elimu na mafunzo kuhusu usimamizi na udhibiti wa kemikali kwa wadau wanaojishughulisha na kemikali kama wajasiriamali.

Alisema lengo ni kuwa na weledi katika matumizi ya kemikali na uelewa wa kutosha kuhusu kemikali na madhara yake ili kuzitumia kwa faida ili kujipatia kipato na wakati huo huo kulinda afya za binadamu na mazingira. "Ni matumaini yangu kuwa mafunzo haya yamebadilisha mitazamo yenu juu ya matumizi ya kemikali na itakuwa chachu kwenu kama wajasiriamali kuzingatia masharti ya matumizi salama ya kemikali," alisema Dk. Mafumiko.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Agnes Kuratha, aliishukuru GCLA kupitia Ofisi ya Kanda ya Mashariki kwa kuandaa mafunzo hayo yenye lengo la kuwajengea uwezo na maarifa zaidi wajasiriamali wanaotumia kemikali katika shughuli zao za kibiashara.


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe | Nipashe mwendo mdundo

Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)

PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store | Google Play

KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz | nipashe | TheGuardiantz | YouTube TheGuardiantz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dar inahitaji mpango kuyaondoa mafuriko

**JUZI** mvua kubwa ilinyesha jijini Dar es Salaam kwa zaidi ya saa 12, na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi, uharibifu mkubwa wa mali, miundombinu na vifo vya watu wanane wakiwamo watoto wawili.

Kutokana na mvua ya siku moja barabara zote za lami na changarawe zilikuwa taabani kutokana na miundombinu kushindwa kuhimili maji ya mvua, kwa mitaro kujaa maji mengi kiasi cha kushindwa kuonekana kingo zake.

Barabara zote za kuingia na kutoka ndani ya jiji zilizidiwa na maji kiasi cha vyombo vya usafiri kama magari yaliingia maji ndani, kuharibika, kingo za madaraja kubomoka, makalavati kuzolewa na maji huku kuta za nyumba zikibomoka na kuta nyingine za fensi za nyumba.

Pia taarifa zinaeleza watu kadhaa walijeruhiwa, na wengine walifika nyumbani usiku wa manane na wengine kuamua kulala sehemu tofauti na nyumbani ili kubaki salama.

Kwa ujumla, mvua hiyo ilionyesha uhalisia wa miundominu ya Jiji la Dar es Salaam kuanzia barabara za ndani na nje katika kubeba maji mengi ya mvua kwa wakati mmoja.

Picha za video zilionyesha magari yalivyokwama, yalivyoingia maji ndani na madereva kutumia vikopo kuchota, baadhi ya nyumba eneo la Jagwani zilifunikwa kabisa na kwingine hakupitiki.

Katika barabara ya Mwenge Morocco ambako ujenzi unaendelea hali ilikuwa mbaya zaidi kwa kuwa miundombinu hiyo mipya hakuweza kumudu maji ya mvua, jambo ambalo linaonyesha bado kuna jambo linatakiwa kufanyika kabla ya kukabidhiwa kwa barabara hiyo.

Kwa barabara za ndani ya makazi ya watu ambazo nyingi ni za kiwango cha changarawe zilikuwa taabani kiasi cha kushindwa kupitika, huku magari yakikwama na kuharibika kwenye maeneo ya mabonde.

Maeneo ya Posta, Muhimbili, Upanga na Mikocheni, Masaki nako hali ilikuwa hivyo hivyo wenye magari walionekana wakitaabika kupita huku magari yakizidiwa na maji na baadhi ya shule maji yakiingia madarasani kiasi cha masomo kuahirishwa.

Eneo la Tegeta na Bunju nyumba nyingi ziliingiliwa na maji, hali inayodhihirisha kuwa miundombinu ya jiji bado inahitaji matengenezo makubwa ili wananchi waishi kwa amani majira yote ya mwaka. Imekuwa kawaida kila kunapokuwa na mvua lazima majanga yatokee, ikiwamo barabara kujaa maji kwa kuwa miundombinu iliyopo haiwezi kumudu maji ya mvua.

Hili ni fundisho kwa makandarasi wanaojenga miundombinu ya barabara kujua kuwa inahitajika miundombinu inayoweza kumudu maji ya mvua nyakati zote na kuyapeleka baharini.

Pia, wapo wananchi waliojenga maeneo yasiyotakiwa kwa maana ni bondeni, kando mwa mito na mkondo wa maji, lakini bado hawaondoki licha ya usumbufu wanaokutana nao kila majira ya mvua. Mvua hii ni ya siku moja na itaendelea zaidi kwa kuwa sasa tunaelekea kwenye miezi ya mvua kila siku, maana yake kila mwananchi achukue tahadhari kuhakikisha wanakuwa salama.

Kwa wajenzi wa miundombinu wahakikishe inajengwa inayomudu maji ya mvua nyakati zote na za ukame pekee, kila nyakati za mvua hali halisi huonekana, lakini bado hali imekuwa ile ile. Ilitarajiwa ujenzi unaofanyika sasa kuendana na hali halisi ya maji ya mvua hasa yanapokuwa mengi, lakini hali ni tofauti.

Pia mvua hizi zinatufundisha kuwa miundombinu ya kwenye makazi ya watu bado kuna kazi kubwa ya kufanya, kwamba inatakiwa kujengwa ili wananchi waweze kupita kutoka eneo moja kwenda jingine.

Hili tatizo linaweza kuisha kabisa ikiwa kunakuwapo na mpango mkakati wa kuliboresha Jiji la Dar es Salaam; kubwa zaidi ni kutengwa fedha katika bajeti za kila mwaka kwa ajili ya kujenga mfumo imara wa mifereji ya kuelekeza maji yanapotakiwa kwenda (baharini).

Kadhalika, sheria zilizopo zitumike kuwadhibiti wale wote wanaojenga kiholela bila kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za ujenzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Mvua ilivyovuruga wakazi Dar, suluhisho lake sasa litafutwe

Na Beatrice Moses, TUDARco

**OKTOBA** 13 mwaka huu inaingia katika kumbukumbu ya aina yake kwa wakazi wengi wa Dar es Salaam, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha na kuvuruga kwa namna moja au nyingine ratiba za kila siku za wakazi.

Mvua hiyo ilikuwa sababu tosha kuvuruga ratiba za watu wengi jijini, kwani ghafla walijikuta wakihamia maisha ya kijijini pasipo kupenda, wakatambua kumbe wana uwezo wa kutembea mwendo mrefu kuelekea kwenye makazi yake.

Kwa kawaida, wasio na magari hupatwa na wakati mgumu kutokana na kusaka usafiri wakitamani japo kupewa lifti na wenye magari, juzi ikawa ya ajabu.

Walitamani wajitwishe kichwani vyombo hivyo vya moto, ili nao waunganishe mwendo kwa miguu kutokana na foleni ya aina yake iliyotokea katika takriban maeneo yote jijini. Nilikuwa miongoni mwa waandamanaji wa hiari wa mvua hiyo. Kama mzazi, nilijikuta nalazimika kuwafuata watoto wangu waliokwama na wenzao, baada ya miundombinu ikiwamo baadhi ya madaraja na barabara kubwa kujaa maji, hivyo kuwekwa vizuizi maalum. Ni hatua ya kuzuia athari za kusombwa na maji.

Imezoeleka, wakazi wa vijijini wanamudu utembeaji mwendo mrefu, kulingana na hali duni ya miundombinu na makazi wanayoishi.

Kilichojiri juzi jijini Dar es Salaam, nilibaini maisha yalibadilika ghafla, kwa kuwasikia baadhi ya wenye magari yakiwamo ya kifahari, wanatamani kuungana na wakazi wengine kutembea, lakini walishindwa. Walikuwa kwenye foleni zilizoganda bila kusogea.

Wenye shida mbalimbali hata wafiwa, walijikuta kwenye wakati mgumu kufanikisha waliyonuia kuyafanya wakati huo. Ratiba za wakazi zilivurugwa haswa!

Hapo ndipo panapozaa funzo kubwa kwa waumini wa Mwenyezi, kwamba anamiliki ratiba na nyendo za dunia.

Kwa upande wa serikali, naamini kichojiri jana kimeifungua serikali macho kuhusu kinachoendelea, ili kuchukulia hatua marekebisho yanayolenga, kuwaondolea na kupunguza adha husika. Ni wazi kwamba huilo ni gumu kuzuia mvua, lakini inawezekana kudhibiti athari zake.

Huu ni msimu wa uchaguzi utakaozalisha viongozi wenyeji wa maeneo kama vile wabunge, madiwani, ambao ndio mzizi wa kuubuliwa meya na wenyeviti wa halmashauri mbaimbali nchini, wawe wenaojua vyema kinachojiri mitaani kwao.

Ngazi za serikali za mitaa, kuna haja ya kuhakikisha kanuni zinazoruhusu mwenyekiti kutoa adhabu ndogo zenye manufaa kwa jamii anayoiongoza.

Hatua hiyo inapaswa kuchukuliwa kwa kuwa, kuna baadhi ya wananchi wakaidi hawapendi kushiriki kwenye shughuli zinazowahusu kwa namna moja au nyingine, kama vile usafi wa mazingira, kuboresha au kukarabati barabara za mitaa zilizoharibika, kusafisha mirefeji ambayo kwa ujumla zina maana kubwa dhidi ya msimu wa mvua na athari zake.

Kuna walio hodari kulalamika, lakini hawatambui kabisa kwamba hakuna fungu la fedha liliotengwa kwenye bajeti linaloweza kutumika kulipa vijana waweze kufaya kazi hizo nilizozitaja.

Kanuni zinaweza kuwека wazi kuwa, mwananchi anaweza kuchagua kuchanggia nguvu kazi au mali ili kufanikisha utendaji kazi za muhimu kwa jamii.

Inajulikana kuwa 'Umoja ni Nguvu' sasa mwananchi asiyetaka umoja, kanuni zinapasa kumbana awajibike na kutambua faida ya umoja huo.

Hapo ni pamoja na kukarabati au kufanyia usafi wa miundombinu iliyopo kwenye maeneo husika hadi wakati bajeti itakapotosheleza na kuwawezesha watu mitaani, kuajili watu maalum kwa kazi hiyo.

Mafuriko ndani ya Dar es Salaam, yanachangiwa na mengi, ikiwamo kutofanyika usafi kwenye miundombinu mbalimbali.

Pia kuna wakazi wachafuzi wa mazingira wanaotupa taka ngumu mtoni na miferejini, kwa imani kwamba yatasombwa, lakini kumbe anarundikana na kusababisha njia ya maji kuzibwa. Kwa kuwa yana nguvu, huwa yanapasua njia tofauti matokeo ya kusababisha madhara na usumbufu mkubwa kwa jamii, kama ilivyotokea juzi.

Naamini wenyeji wa jiji wanaweza kuwa na kumbukumbu nzuri kuwa, kuna namna tatizo linakuwa hali kuwa ya kawaida msongamano wa magari, lenginme kama Jangwani, katika hatari ya kusombwa na maji.

Niseme, pamoja na maboresho ya kanuni za sheria ndogo za utunzaji mazingira, viongozi wa mitaa nchini wanawajibika kuhakikisha wanadhibiti uharibifu. Katika baadhi ya maeneo mengi kumekuwapo adha kubwa ya uchafuzi wa mazingira, kiwango cha kushangaza licha ya kuwapo sheria zinazowabana wahusika. Baadhi ya viongozi wa mitaa wanafumbia macho yanayochochea madhara namna hiyo kwa jamii.

# Katika Kuadhimisha Miaka 55 ya Utiaji Saini Mkataba wa Urafiki kati ya China na Tanzania

# Kuimarisha Urafiki wa China na Tanzania Kufikia Maendeleo ya Pamoja



**Mhe. Wang Ke, Balozi wa China nchini Tanzania**

Oktoba 14, 2020 inatimiza miaka 21 ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, tangu alipofariki dunia. Katika hafla ya kuomboleza kifo chake, tunakumbuka kwa hisia kali mafanikio makubwa yaliyofanywa na viongozi wa kizazi cha wazee wa nchi zetu mbili katika kuanzisha harakati ya urafiki kati ya China na Tanzania, na kuamua kuendeleza urafiki huo kwa kuandika sura mpya ya ushirikiano kwa faida ya nchi zetu mbili.

Mwaka wa 1965 una umuhimu wa kipekee katika historia ya uhusiano kati ya China na Tanzania. Matukio makubwa matatu yalitokea mwaka huo, ambayo ni ziara ya kwanza ya serikali ya Rais Julius Nyerere nchini China, kutiwa saini kwa Mkataba wa Urafiki kati ya China na Tanzania, na ziara rasmi ya Waziri Mkuu Zhou Enlai nchini Tanzania. Hafla hizo tatu za kihistoria zilichangamsha sana uhusiano wa nchi hizi mbili ambao ulikuwa na mwaka mmoja tu, na kuanzisha msingi thabiti wa urafiki wa nyakati zote kati ya China na Tanzania na ushirikiano mzuri.

Februari 1965, Rais Julius Nyerere alifanya ziara yake ya kwanza ya kiserikali nchini China, ambayo ina umbali wa maelfu ya maili. Alikaribishwa kwa uchangamfu na kupokelewa na viongozi wa zamani wa China, kama Mao Zedong, Zhou Enlai na Liu Shaoqi, na watu wa China. Kupitia ziara hii, Rais Nyerere aliunda urafiki mkubwa wa kibinafsi na viongozi wa China. Alijaribu kutoa ombi la msaada kutoka China la kujenga Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), na bila kutarajia, viongozi wa China walimpa majibu mazuri licha ya ukweli kwamba China ilikua masikini wakati huo. Mwenyekiti Mao Zedong alimwambia Rais Nyerere, "Una shida, sisi pia tunazo. Lakini shida zako ni tofauti na zetu. "Bado tutakusaidia kujenga reli hii hata ikiwa inamaanisha kuwa hatutaweza kujenga reli kwenye ardhi yetu wenyewe." Kwa furaha yake, Rais Nyerere alipata nchi licha ya kuwa mbali, inayoichukulia Tanzania kama mshirika sawa na kuwa tayari kutoa msaada wa dhati. Kwa sababu hiyo, Rais Nyerere alifanya nia yake ya kukuza uhusiano na China. Alikuwa amejitolea kuimarisha uhusiano wa kirafiki kati ya China na Tanzania na China na Afrika katika maisha yake yote. Alitembelea China kwa mara 13, ambayo ilimfanya kuwa mmoja wa wakuu wa nchi za kigeni ambao walitembelea China mara nyingi. Julai 1, 1997, Mwalimu Nyerere, ambaye tayari alikuwa mzee wakati huo, alikubali mwaliko wa China kwa furaha kuhudhuria hafla ya kukabidhi Hong Kong, na alitoa pongezi za dhati kwa watu wa China waliotimiza matakwa yao ya muda mrefu.

Mafanikio mengine muhimu ya ziara ya Rais Nyerere nchini China mwaka 1965 ni kutiwa saini kwa Mkataba wa Urafiki kati ya China na Tanzania. Huu ni mkataba wa kwanza wa urafiki ambao China imesaini na nchi iliyoko Mashariki na Kusini mwa Afrika. Kwa hivyo imechukua jukumu muhimu la kuongoza na la mfano katika maendeleo ya uhusiano kati ya China na Afrika. Mkataba huo mwanzoni unasema, "Kuimarika kwa ushirikiano wa kirafiki kati ya China na Tanzania kunalingana na maslahi ya kimsingi ya watu wa nchi hizi mbili, inasaidia kukuza mshikamano kati yao na pia na watu wa Asia na Afrika na mapambano ya pamoja dhidi ya ubeberu na inaleta amani katika Asia, Afrika na ulimwenguni". Kanuni tano za kuishi pamoja kwa amani, ari ya usawa, faida kwa wote na ushirikiano wa kirafiki, na kusuluhisha suala lolote kwa njia ya mashauriano ya amani, kama ilivyoainishwa katika Mkataba, ndio kanuni muhimu za kudumu ambazo zimehakikisha maendeleo thabiti na mazuri ya uhusiano kati ya China na Tanzania.

Wakati wa ziara yake nchini China, Rais Nyerere alitoa mwaliko wake wa dhati kwa viongozi wa China kufanya ziara nchini Tanzania. Kama taifa linaloangazia umuhimu wa heshima na urafiki, watu wa China hawakuwavunja moyo marafiki zao. Miezi minne baada ya ziara ya Rais Nyerere nchini China, Waziri Mkuu, Zhou Enlai alifanya ziara ya kurudi nchini Tanzania. Umati wa watu wa Tanzania kwa hiari yao walimiminika barabarani kumkaribisha Waziri Mkuu Zhou, na lilikuwa tukio la kushangaza. Wakati wa ziara hiyo, Rais Nyerere alisema, na ishara za kutayarisha, Tanzania ilibidi kwanza ichunguze uwezekano wa kupata misaada kutoka nchi za Magharibi kujenga TAZARA, Waziri Mkuu Zhou alijibu kwa ukarimu, "Haijalishi ni nani anayejenga TAZARA. Lazima ijengwe mapema iwezekanavyo. Ikiwa nchi za Magharibi hazitaki kuijenga, China itaijenga. Kwa ruhusa, Mheshimiwa anaweza kujadiliana na nchi za Magharibi." Rais Nyerere aliguswa sana na maneno haya. Hekima, upole na urafiki wa Waziri Mkuu Zhou uliwavutia sana Watanzania, na baada ya ziara hiyo jina "Zhou Enlai" likajulikana kwa Watanzania. Wakati Waziri Mkuu Zhou alipofariki dunia mwaka 1976, watu wa Tanzania walihisi huzuni kubwa sawa na Wachina. Wengi wao walikuja kwa Ubalozi wa China kuomboleza Waziri Mkuu Zhou, na foleni ilikuwa na urefu wa kilomita kadhaa. Katika barua yake ya rambirambi, Rais Nyerere aliandika kwamba Waziri Mkuu Zhou Enlai ni mtu mashuhuri wa China na ulimwengu wote, kwamba watu wa Tanzania wanamchukulia kama mtu mashuhuri, rafiki mkubwa wa wanadamu na kiongozi anayehamasisha wengine, na kwamba Watanzania wanaguswa na maoni yake mapana na ya kina, na kujitolea kwake kwa uhuru, haki na amani ya kimataifa.




*Waziri Mkuu wa China, Zhou Enlai, akiwasili jijini Dar es Salaam kwa ziara ya kiserikali nchini Tanzania, akipokewa na mwenyeji wake Rais Julius Nyerere, uwanja wa ndege, Juni 4, 1965. PICHA: XINHUA*

Licha ya mabadiliko ya haraka na makubwa ulimwenguni katika kipindi cha miaka 50 iliyopita na zaidi, udugu usiovunjika kati ya China na Tanzania na imani yao thabiti ya ushirikiano wa kirafiki bado haujabadilika. Mwaka 2013, wakati Rais Xi Jinping wa China alipofanya safari yake ya kwanza ya nchi za nje baada ya kuchukua urais, alikuja Afrika, na Tanzania ilikuwa kituo chake cha kwanza. Katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, kilichojengwa kwa msaada wa China, Rais Xi Jinping, alipendekeza kanuni ya uaminifu, matokeo halisi, uhusiano mwema na imani nzuri, na kanuni ya kufuata maslahi makubwa na ya pamoja kwa mara ya kwanza. Dhana hizi zilifafanuliwa kama kanuni elekezi za China katika uhusiano wake na nchi zinazoendelea katika Kongresi ya 19 ya Kitaifa ya Chama cha Kikomunisti cha China, ambayo inaonyesha kuwa uhusiano wa China na Tanzania uko mbele katika uhusiano wa nchi hiyo na Afrika na ushirikiano wa nchi za Kusini .

Kwa miaka 50 iliyopita na zaidi, China na Tanzania zimekuwa zikiheshimiana na kusaidiana kila mara. Nchi hizi mbili zinaheshimu haki ya kila mmoja kuchagua kwa uhuru mfumo wa kisiasa na njia ya maendeleo, na bila shaka zinaunga mkono juhudi za kila mmoja kulinda uhuru wa kitaifa, usalama na maslahi ya maendeleo. Mwanzoni mwa kuanzishwa kwa uhusiano wa kidiplomasia, China ilisaidia Tanzania kutoa mafunzo kwa wapigania uhuru, iliunga mkono Tanzania katika ujenzi wa taifa, na ilitoa msaada muhimu kwa Tanzania na nchi zake jirani katika kuimarisha majimbo mapya. Mwaka 1971, Tanzania ilitoa michango muhimu ya kurudisha kiti halali cha China katika Umoja wa Mataifa. Katika hafla ya kuadhimisha miaka 70 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa China, Waziri Mkuu wa zamani wa Tanzania, Dk. Salim Ahmed Salim, ambaye alikuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania kwa UN tangu 1970 hadi 1980, alipewa Nishani ya Urafiki na Rais Xi wa China Jinping, na hivyo kuwa mpokeaji pekee wa Kiafrika wa heshima kubwa zaidi ya China kwa wageni. Mwaka huu (2020), wakati dunia ikikabiliwa na mlipuko wa ghafla wa ugonjwa wa COVID-19, China na Tanzania kwa mara nyingine waliungana na kushirikiana bega kwa bega. Wakati mgumu zaidi katika vita vya China dhidi ya janga hilo, Serikali ya Tanzania na watu kwa wakati walionyesha huruma yao na kutoa msaada wao wa dhati kwa China. Baada ya Tanzania kuathiriwa na COVID-19, China ilianza kutoa msaada mapema iwezekanavyo, na nchi ya kwanza kusaidia kupamba na ugonjwa huo ni Tanzania.

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita na zaidi, ushirikiano kati ya China na Tanzania umekuwa na faida pande zote, heshima na ari ya kushinda. Nchi hizi mbili zimefanya ushirikiano wenye tija katika miundombinu, viwanda, kilimo, biashara, uwekezaji, elimu, afya, utalii, n.k China imekuwa mshirika mkubwa wa kibiashara wa Tanzania kwa miaka minne mfululizo. Mwaka 2019, kiwango cha biashara kati ya nchi hizo mbili kilizidi Dola za Kimarekani bilioni 4.1, ikishika nafasi ya pili katika biashara baina ya China na nchi za Afrika Mashariki. China ndio chanzo kikuu cha uwekezaji kwa Tanzania, na zaidi ya miradi 700 na jumla ya thamani inayozidi Dola za Kimarekani bilioni saba. Miradi hii ya uwekezaji imetengeneza takribani ajira 150,000 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa Watanzania. Ushirikiano kati ya China na Tanzania umeunda miradi mingi "mikubwa" na "ya kwanza". Reli ya Tanzania na Zambia ni mradi mkubwa zaidi wa msaada wa nje ambao China imewahi kufadhili na kuifanya nje ya nchi tangu kuanzishwa kwake mwaka 1949. Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndio maktaba kubwa zaidi ya kisasa barani Afrika iliyojengwa kwa msaada rasmi wa China. Miongoni mwa miradi mingi inayofanywa na kampuni za Wachina, Daraja la Nyerere ni daraja la kwanza linalopita juu ya maji katika Afrika Mashariki. Flyover ya Ubungo inayokamilika hivi karibuni itakuwa mabadilishano ya hali ya juu zaidi nchini Tanzania. Kwa miongo mitano iliyopita, China imekuwa ikituma timu za matibabu, wataalam wa jeshi na wataalam wa kilimo kufanya kazi na watu wa Tanzania, na wamekuwa "mabalozi wa nia njema" kati ya nchi zetu mbili.

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita na zaidi, China na Tanzania zimedumisha mabadilishano kwa karibu kati ya watu na watu. China imeipatia Tanzania udhamini wa masomo wa serikali karibu 2,000 na karibu fursa 7,000 za mafunzo ya muda mfupi. China inakuwa mahali maarufu kwa vijana wa Kitanzania kusoma na kufanya kazi. Tangu kuzuka kwa COVID-19, China imekuwa ikilinda Watanzania kama raia wake, na vyuo vikuu vya China na walimu wameangalia karibu wanafunzi 5,000 wa Kitanzania nchini China kama watoto wao,

INAENDELEA UK 9.

# Katika Kuadhimisha Miaka 55 ya Utiaji Saini Mkataba wa Urafiki kati ya China na Tanzania

## Uhusiano wa Tanzania na China Tangu Mwanzo wa Mkataba wa Urafiki



*Na Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi Waziri wa mambo ya nnje na ushirikiano wa Africa Masharik*

Mwaka huu ni muhimu kwa uhusiano wa nchi mbili kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China, tunaposherehekea miaka 55 tangu kutiwa saini kwa Mkataba wa Urafiki kati ya Tanzania na China mnamo 1965. Mkataba ambao uliunda maadili ya msingi ya urafiki wetu ushirikiano na mshikamano. Kwa kila jambo, hii ni hatua muhimu ya urafiki wetu wa kihistoria na wa hali na mali. Urafiki ambao unasimamia maadili ya kuheshimiana, usawa wa enzi kuu na kutokuingiliana katika mambo ya ndani ya kila mmoja.

Tunapoheshimu Waanzilishi wa Mkataba huu, ambao ni hayati Mwalimu Julius Nyerere na marehemu Mwenyekiti Liu Shaoqi, Tanzania ingependa kurudia kujitolea kwake kudumisha na kukuza uhusiano wa amani na urafiki sio tu kwa kufuata Mkataba, lakini pia sambamba na ushirikiano kamili wa kimkakati uliosisitizwa na Mpango wa Ukanda na Barabara (BRI) na Jukwaa la Ushirikiano wa China na Afrika (FOCAC).

Inafaa hafla hii kukumbuka kile Mwalimu Nyerere alichosema wakati wa ziara yake kuu ya kitaifa nchini China mnamo tarehe 26 Februari 1965, ziara hiyo ambayo ilishuhudia kutiwa saini ya Mkataba tunaousherehekea leo wakati alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara wa maelfu ya watu huko Beijing alisema kwamba:

*"Tunataka kuwa na urafiki na wote, na kamwe hatutawaruhusu marafiki wetu kutuchagulia maadui zetu. Ni kufuata mafundisho haya kwamba Tanzania inafurahi sana katika urafiki wake mpya na China. Sasa tuna rafiki, na mkubwa, rafiki mpya, na rafiki ambaye tulizuiliwa kutoka naye siku za ukoloni. Hofu ya wengine haitaathiri urafiki wa Tanzania na China, kama vile urafiki wetu na nchi zingine hautaathiriwa na kile wapinzani wao wanasema juu yao. "*

Kwa kweli, msaada wa China kwa Tanzania tangu kusainiwa kwa Mkataba huo, miongo mitano iliyopita hauna kipimo. China imetoa msaada kwa Tanzania kutekeleza miradi mbali mbali katika nyanja zote ikiwa ni pamoja na afya, ulinzi na usalama, kilimo, miundombinu, elimu na sekta za viwanda. Miradi hii imechangia sana maendeleo na ustawi wa Watanzania, ikithibitisha wazi kuheshimiana na urafiki ambao upo kwa furaha kati ya nchi zetu hizi mbili.

Moja kati ya hatua kubwa za uhusiano kati ya Tanzania na China ni ujenzi wa reli ya urefu wa kilometa 1,868 kati ya reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) pia inajulikana kama reli ya UHURU. Ombi hilo kwa Mwenyekiti Mao Zedong, kujenga TAZARA lilitolewa kwa pamoja na hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, baba wa Taifa letu na Daktari Kenneth David Kaunda, Rais wa zamani wa Jamhuri ya Zambia, wakati wa vita baridi. Ilifanywa wakati Zambia, nchi isiyo na bandari na nchi mpya iliyojitegemea ilikuwa imezungukwa na tawala zenye uhasama ambazo zilimnyima ufikiaji wa bahari na njia salama tu baharini ilikuwa kupitia Tanzania. Hivi ndivyo China ilikuwa tayari kusaidia mapambano ya watu wa Afrika kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Msimamo huo wa China umeendelea kuwa thabiti hata leo.

Mifano mingine inayoangazia ushirikiano wetu wa kiuchumi katika hatua ya awali ya urafiki wetu ni pamoja na kuanzishwa kwa Kiwanda cha Nguo cha Urafiki kati ya Tanzania na China (URAFIKI), Ubungo Farm Vifaa (UFI), Viwanda vya Keko vya Dawa, Kiwanda cha Sukari cha Mahonda huko Zanzibar, kusaidia mpango wa umwagiliaji Ruvu katika Mkoa wa Pwani na shamba la mpunga la Mbarali jijini Mbeya. Hii ilifanywa na China kutii wito wa mipango ya viwanda nchini Tanzania katika nguo, kilimo na dawa.

Kwa hilo na mengine mengi, Tanzania ilifurahi sana wakati Jamhuri ya Watu wa China ilipoingia tena Umoja wa Mataifa mnamo 1971. Tanzania iliunga mkono Jamhuri ya Watu wa China kuandikishwa tena kwa Umoja wa Mataifa kwani tuliamini kutengwa kwake kunapunguza sana ufanisi ya Umoja wa Mataifa katika utoaji wa agizo lake la kuunganisha nguvu ya kudumisha amani na usalama wa kimataifa.

Katika miaka ya hivi karibuni, uhusiano wa Sino na Tanzania umebadilika kuwa uhusiano wa kisasa na wa vitendo na ushiriki mkubwa na anuwai wa uchumi katika biashara, miradi ya miundombinu, na uwekezaji. China inabaki kuwa mshirika mkubwa wa kibiashara wa Tanzania, na 19.3% ya bidhaa zilingia Tanzania kwa mwaka 2017/2018 kutoka China. China pia ni chanzo kikubwa zaidi cha Uwekezaji wa moja kwa moja wa Kigeni (FDI) na hisa ya uwekezaji wa miradi zaidi ya 700 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 7.1 na kutengeneza ajira zaidi ya themanini na saba elfu (87,000).

Tunapojitahidi kukamilisha haraka safari za ndege za moja kwa moja za Air Tanzania (ATCL) kutoka Dar es Salaam kwenda Guangzhou na kufungua Ubalozi Mdogo wa Tanzania huko Guangzhou, China, tuna hakika kuwa hii itaboresha na kuimarisha uhamaji wa watu, mwingiliano wa kibiashara na utalii sio tu kati ya China na Tanzania bali pia kati ya China na Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Tanzania inabaki kuwa msaidizi thabiti wa FOCAC na BRI kwani vipaumbele vyao vikuu vinalingana kabisa na Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025 iliyoongozwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli, kiini cha ajenda zote ni kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia viwanda. Tunapoendelea kufaidika mara kwa mara na msingi wa pamoja wa masomo, mafunzo ya muda mfupi, kujenga uwezo, ushirikiano wa kitamaduni, kubadilishana maarifa, utafiti, na ubadilishanaji wa watu kwa watu unaotolewa na China, Tanzania inaendelea kushawishika kwamba, pamoja na juhudi za pamoja ushirikiano wetu wa elimu utaimarishwa zaidi na kushamiri kwa kuhusisha mafunzo ya kazini, kufikiria kwa kina, utatuzi wa shida, ugunduzi, na mafunzo ya uzoefu.

Sherehe ya miaka 55 ya urafiki inakuja wakati ulimwengu wote unapambana na janga lenye changamoto kubwa ya COVID-19. Tanzania haikukwepa kupata maambukizi haya. Katika vita vyetu dhidi ya janga hili, tuliamini katika mkakati wa "vita vya pamoja", tukitaka kuzingatia maadili ya kitaifa ya umoja, mshikamano, sala na amani.

Ingawa katika kila hali maadili haya ya kitaifa yanabaki muhimu katika vita yetu dhidi ya janga hilo, itakuwa uzembe kwetu kutokubali Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ushawishi wake ambao ulisababisha uamuzi wa Viongozi wa G20 kusitisha ulipaji wa deni kwa nchi zilizoendelea kidogo ikiwemo Tanzania.

Usaidizi huu utaturuhusu kuzima athari mbaya za kiuchumi zinazosababishwa na COVID-19. Sisi pia, tunathamini utayari wa China kutoa msaada ili kuongeza utayarishaji wa matibabu wa nchi zingine zilizoathirika. Hii inaonyesha kikamilifu ukarimu wa kipekee wa China na uwezo katika kushughulikia dharura za afya ya umma kwa kuweka masilahi ya watu mbele.

Kwa kifupi, hii ndio njia ambayo mtu anaweza kuonyesha uhusiano kati ya Tanzania na China katika miaka 55 iliyopita. Safari ambayo tumepitia, haiba zilizounda uhusiano, hatua muhimu zilizopatikana katika uhusiano wetu na changamoto ambazo tumeshinda, zinapaswa kutumikia kutukumbusha haswa kizazi kipya ambapo tumefika. Vitu ambavyo kizazi kipya lazima kiige kutoka kwa waanzilishi wa uhusiano huu ili kuendeleza ari yake na kuifanya iendelee.



*Rais Julius Nyerere na Mwenyekiti Liu Shaoqi, wakisaini mkataba wa urafiki kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China, Beijing, Februari 20, 1965: PICHA XINHUA*

## Katika Kuadhimisha Miaka 55 ya Utiaji Saini Mkataba wa Urafiki kati ya China na Tanzania

# Ziara ya Waziri Mkuu Zhou Enlai nchini Tanzania ilikuwa ni historia katika Maendeleo ya Tanzania



*Na Mh. Job Lusinde, waziri wa zamani Mambo ya Nje, Tanzania*

Ziara ya Waziri Mkuu wa China nchini Tanzania ilikuwa ni historia katika maendeleo ya uhusiano mwema kati ya nchi zetu mbili. Miradi kadhaa iliyosaidiwa na Serikali ya China nchini Tanzania ilikuwa tayari imeanza kwa kipindi kile. Hivyo, urafiki kati ya Tanzania na China ulianza kabla ya Waziri Mkuu Zhou Enlai kutembelea Tanzania. Mtakumbuka kwamba mwaka 1964, jeshi letu liliasi na ilikuwa lazima kulivunja na kuanza kujenga jipya. Serikali ya China ilitupatia vifaa bure vilivyohitajika kulipa nguvu jeshi letu. Zaidi, serikali ya China ilitusaidia kutoa mafunzo kwa jeshi la polisi, na Moshi, walibomoa majengo makuu kuu ya shule na kujenga mengine zaidi yanayofaa kwa ajili ya chuo. Ziara ya Zhou haikuwa kuona wanyama na kufurahia vivutio vya utalii. Alikuja kufanya ukaguzi wa kazi iliyokuwa imefanywa kwa msaada wa China, na kujadili masuala yenye maslahi kati ya nchi zetu mbili.

Waziri Mkuu Zhou Enlai alipokelewa na kundi la watu wakiwa na shauku ambayo lilikuwa haijawahi kuonekana Dar es Salaam. Kuna sababu kadhaa, kwanza ilikuwa kwamba, kulikuwa na propaganda nyingi dhidi ya China kutoka kwa nchi za Magharibi ambazo zilitufanya tuwe na huruma kwa China, nchi ambayo pia iliyofanyiwa udhalimu kutoka nje, na ikapigania ukombozi. Pili, watu wa Tanzania walisikia mambo mengi mazuri kuhusu Waziri Mkuu Zhou, hasa kama mmoja wa waasisi wa sera ya kutofungamana na upande wowote, ambayo ilikuwa msingi wa Sera ya Mambo ya nje ya Tanzania. Na mwisho, ingawa wakati ule hatukuwa tumetengeneza vizuri mawazo yetu ya ujamaa, Misingi ya Chama Cha Tanganyika African National Union (TANU, na chama tawala cha Tanzania bara wakati ule), zilikuwa na mwelekeo wa ujamaa. Watu walihitaji kumuona kiongozi wa nchi kubwa ya kijamaa ya China.

Niliteuliwa kumsindikiza Waziri Mkuu Zhou Enlai wakati wote wa ziara yake. Ilikuwa ni heshima kubwa kwangu kusafiri naye mahali pote. Nilikuwa Waziri wa Mambo ya Nje. Waziri Mkuu Zhou alikuwa ni mtu rafiki sana. Aliweza, ndani ya muda mfupi, kukufanya uwe na amani na kujisikia uko vizuri katika kuwa naye. Mwalimu Nyerere alikuwa pia na kipaji hicho. Alikuwa muda wote akikufanya kujisikia kuwa na amani. Waziri Mkuu Zhou alituzungumzia kirafiki kuhusu China - kuhusu matatizo na magumu waliyokumbana nayo na namna walivyopanga kukabiliana nayo. Wakati Mwalimu na Waziri Mkuu Zhou wakiwa wanazungumza, walicheka mara nyingi, ungeliweza kuona kwamba, hakika walipendana, na ilikuwa inafurahisha kuwaona.

Waziri Mkuu Zhou alikuwa akifahamika kama msomi na mtu mwenye akili sana. Alifahamu siasa za dunia vizuri sana, na alikuwa na hakika na takwimu za masuala mengi katika vidole vyake. Alikuwa pia na kumbukumbu nzuri na aliweza kukumbuka pia hata taarifa ndogondogo kuhusu mada zote. Alikuwa pia na uelewa na msimamo wa China katika ulimwengu na aina ipi ya nchi inahitaji kuwa.

Jambo moja muhimu lililochochea uhusiano wetu na China, ilikuwa kwamba, kutoka wakati Tanganyika ilipopata uhuru, ilifuata msimamo wa Jamhuri ya Watu wa China (PRC), kuwa haikutakiwa kuwa nje ya Umoja wa Mataifa, wakati Taiwan ikidai kuiwakilisha China yote. Tanzania kamwe haikusita kuunga mkono kurejeshwa kwa PRC kwenye nafasi yake katika UN. Serikali ya China na viongozi wake walifurahishwa na msimamo huu uliochukuliwa kama suala la msingi na hali.

Mijadala kuhsu ujenzi wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), ilikuwa ikiendelea wakati huo. Mwalimu Nyerere alikuwa tayari ameshatembelea China na kukutana na Mwenyekiti Mao Zedong na Waziri Mkuu Zhou Enlai. Baada ya Mwalimu kutoa ombi la msaada wa ujenzi wa TAZARA, Mwenyekiti Mao alimuuliza, 'Je reli itasaidia katika ukombozi wa Africa? Alijibu, 'Ndiyo, itasaidia', Mwenyekiti Mao,' alijibu kwa maneno mafupi manne. 'Itajengwa.' Akisema uwepo wa Waziri Mkuu Zhou ulitoa uhakika kuwa itafanyika kama ilivyoahidiwa. Hicho ni kitu kimoja tulichojifunza. Mwenyekiti Mao alichukua maamuzi ya sera na ilikuwa Zhou aliyemuamini kuyatafsiri na kuyatekeleza kikamilifu.

Ziara yake nchini kwetu, ilikuwa, hivyo basi, sababu muhimu na fursa kujadili maeneo yote ya mradi wa TAZARA ilikuwa ni mradi mkubwa uliotekelezwa na Serikali ya China, nje ya China. Hata kama kwa juu juu, mradi ulikuwa ni ujenzi wa kawaida wa mradi, kiuhalisia, ilikuwa ni zaidi ya hilo. Ilikuwa ni kipindi cha Vita Baridi. Kulikuwa na masuala mengi ya kisiasa, uchumi, kijeshi, na ulinzi yanayopaswa kufikiriwa. Kwa namna gani nchi za Magharibi zilizokataa kuunga mkono zingeichukua? Kwa namna gani mzigo wa kifedha ungeweza kugawanywa na nchi tatu? Kwa namna gani Watanzania wangeweza kutazama uwepo wa Wachina maelfu katika nchi yao? Kwa namna gani wafanyakazi Wachina na Tanzania wangeweza kufanya kazi pamoja, na namna gani usalama wa wafanyakazi ungeweza kuhakikishiwa? Kama Waziri wa Mambo ya Nje, nilishirikishwa kwa kina katika majadiliano haya na mipangilio. Suala ya usalama ni sehemu muhimu zaidi. Nilisema awali, kulingana na tulivyojifunza, Mwenyekiti Mao alimuamini Waziri Miuu Zhou kusimamia miradi yote muhimu ndani na nje ya China. Akili nyingi za kiutawala za Waziri Mkuu Zhou zilikuwa za kishujaa na zilionekana wakati wote wa ujenzi wa TAZARA. Alikuwa mtu wa vitendo sana na alifuatilia kila hatua ya kazi, akitoa miongozo kwa vitendo na hasa katika kuhakikisha usalama na ushirikiano wa juu zaidi miongoni mwa wafanyakazi wa nchi tatu zilizokuwa zikijenga TAZARA.

Nina kumbukumbu nzuri ya Waziri Mkuu Zhou Enlai. Ziara yake nchini Tanzania ilikuwa ni alama ya manufaa ya wote kwa urafiki wa Tanzania na China.

***(Makala hii ni simulizi ya Hayati Job Lusinde kuhusu ziara ya Waziri Mkuu Zhou Enlai Juni 1965, wakati akihojiwa na Bwana Walter Bhoya, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Wachapishaji ya Mkuki na Nyota tarehe 27 Machi 2019)***



*Waziri Mkuu wa China, Zhou Enlai akitoa zawadi kwa mwanachama wa Tanganyika African National Union (TANU), alipotembelea makao makuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam, Juni 7, 1965. PICHA: MAELEZO*

INATOKA UK 7.

na kwa sababu hiyo hakuna hata mmoja aliyeambukizwa virusi. Katika miaka ya hivi karibuni, idadi kubwa ya raia wa China wamekuja Tanzania kwa biashara, masomo, uwekezaji na utalii. Inaaminika kwamba kwa udhibiti wa COVID-19 na kuboreshwa kwa hali hiyo, mabadilishano ya kitamaduni na watu kati ya nchi zetu mbili yatarejea katika hali ya kawaida na kupata nguvu zaidi.

Katika kipindi cha miaka 50 na zaidi, China na Tanzania zimefanya kazi pamoja kusimamia usawa na haki. Nchi hizo mbili zimekuwa wakili mtetezi na mhamasishaji wa ari ya Mkataba wa UN. Tumekuwa tukishikilia sana bendera ya amani, ushirikiano na haki katika masuala ya kimataifa, tukifanya kazi pamoja kulinda maslahi ya jumla ya nchi zinazoendelea, na kufanya kazi kuufanya utaratibu wa kimataifa kuwa sawa na wenye busara. Kwa sasa, mbele ya kuongezeka kwa dola moja kuwa juu ya nyingine, upande mmoja na nguvu ya kisiasa. China na Tanzania zinadumisha mawasiliano, uratibu na ushirikiano wa karibu katika hafla za kimataifa, na hivyo kuwa nguvu muhimu katika kukuza ujamaa na kusimamia mfumo wa pande nyingi. Tanzania imezungumza na China kwa njia anuwai na imeeleza kuunga mkono kwake kwa nguvu juu ya masuala yanayohusu maslahi ya msingi ya China kama vile Taiwan, Hong Kong, Xinjiang na haki za binadamu, ambayo China inashukuru sana.

Kwa sasa, China na Tanzania ziko katika hatua muhimu ya maendeleo yao. China iko karibu kuondoa umaskini kabisa na kukamilisha ujenzi wa jamii yenye ustawi wa wastani kwa njia zote. China inachukua hatua thabiti zaidi kuelekea "Ndoto ya Wachina" ya ufufuo mzuri wa kitaifa. Tanzania iliingia kwenye kundi la uchumi wa kati miaka mitano kabla ya muda uliopangwa, na inafanya kazi bila kuchoka kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2025 na uhuru wa kiuchumi. Katika kipindi kipya cha kihistoria na mbele ya fursa mpya za kihistoria, China na Tanzania zitasaidiana katika maendeleo kwa kila mmoja kwa kufuata utamaduni wa urafiki na ari ya ushirikiano kama walivyofanya kwa zaidi ya miaka 50. China itachukua fursa zilizoletwa na utekelezaji wa matokeo ya Mkutano wa Beijing wa FOCAC na Mkutano wa China na Afrika juu ya mshikamano dhidi ya COVID-19, itaunganisha Mpango wa ukanda na barabara na utekelezaji wa mkakati wa maendeleo wa Tanzania, kuendelea kuimarisha mawasiliano ya sera uratibu wa kimkakati, na kuendelea kubadilishana uzoefu wa utawala na maendeleo na Tanzania. Pia itapanua ushirikiano wa vitendo na Tanzania katika nyanja mbali mbali ili kukuza biashara na uwekezaji, kuimarisha ushirikiano katika miundombinu, uhamishaji wa teknolojia na maendeleo ya rasilimali watu, ili kuisaidia Tanzania kubadilisha faida zake za rasilimali kuwa kasi ya maendeleo na kuleta fursa zaidi za maendeleo na faida inayoonekana kwa watu wake.

Katika wakati huu wa kukumbukwa, tufuate njia ya urafiki thabiti wa China na Tanzania uliowekwa na Rais Nyerere, Waziri Mkuu, Zhou Enlai na viongozi wengine wa kizazi cha wazee wa nchi zetu mbili, na tufanye kazi kufikia lengo la kupata matokeo zaidi kutoka kwa ushindi pande zote na ushirikiano na maendeleo ya pamoja.

# Tigo yazindua simu mpya ya TECNO T-Smart 4G

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano ya Tigo Tanzania, imetambulisha simu mpya katika soko la simu za mkononi nchini, TECNO T-Smart 4G.

Simu hiyo mpya na ya kisasa itasaidia kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma za kidijitali nchini.

Meneja wa vifaa kutoka Tigo Tanzania, Mkumbo Myonga, alisema jana kuwa TECNO T-Smart 4G ambayo hujulikana sana kama TECNO Kitochi, itawapa wateja wao namna bora ya kutumia huduma za kimtandao kama Facebook, Instagram, WhatsApp, YouTube, barua pepe, pamoja na huduma nyingine zinazopatikana kwenye KaiStore.

Aliongeza kuwa uzinduzi wa simu hii mpya katika soko la simu za mkononi nchini kutaongeza thamani na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini, hivyo kuongeza ubora wa maisha kwa Watanzania wote.

"Pamoja na kuwapa huduma zenye ubora wa hali ya juu wateja wetu na kwa gharama nafuu, simu hii itasaidia kupunguza wimbi kubwa la watu wasioweza kupata huduma za kidigitali nchini kwani ni ya gharama nafuu ikiwa na vigezo na sifa zote za simu janja ya 4G," alisema.

Kwa mujibu wa Myonga, simu hizo mpya sasa zinapatikana katika maduka yote ya kampuni hiyo na kwa mawakala pamoja na wabia wao nchi nzima, pia simu hizi zitapatikana zikiwa na ofa ya Facebook bure kwa miezi 12.

Alisema TECNO T-Smart 4G, ni simu yenye huduma zote kama za simu janja, na inaingia sokoni ikiwa tayari imesheheni apps zote maarufu za mitandao ya kijamii. Ni simu yenye uwezo wa 4G ambayo pia inaweza kufanya kazi kama WiFi kwa kuunganisha mpaka vifaa kumi kwa wakati mmoja.

"Hii ni simu inayotoa huduma zote muhimu na kwa viwango vya juu hususani kwa mteja ambaye hana uwezo wa kununua simu janja au kuhofia simu hiyo kuharibika ndani ya muda mfupi kutokana na aina ya kazi za mteja. Simu hii mpya itakuwa sokoni kwa bei ya Sh. 47,900."

# Waziri ataka elimu matumizi ya mbolea

**Na Christina Haule,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, amewataka wadau wa maendeleo, maofisa ugani na watafiti kuendelea kujipanga kimkakati kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea na pembejeo.

Lengo ni kuwafanya wakulima kutoogopa matumizi ya mbolea kwa madai ya kuua ardhi yao.

Aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika kitaifa wilayani Mvomero mkoani hapa, ambapo alisema ikiwa wakulima watatumia elimu watayopewa na wataalamu wa kilimo waliopo sambamba na matokeo ya utafiti wanayotoa wataweza kuzalisha kwa tija

Mgumba alisema mbolea inapotumiwa kwa usahihi sambamba na kuzingatia kanuni za kilimo bora ni dhahiri kutakuwa na uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na mkulima kupata malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda.

Alisema serikali imeweka maofisa ugani wa vijiji ili waweze kuwaelimisha wakulima juu ya matumizi ya teknolojia mbalimbali za kilimo ili kuongeza uzalishaji na tija sambamba na kuweka vituo vya utafiti wa kilimo katika kila kanda ambavyo wakulima wanapaswa kuvitumia. Aliwaomba wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya kutengeneza mbolea nchini ili kuchangia katika ongezeko la upatikanaji wa mbolea na kupunguza bei kwa wakulima.

Alisema kuanzishwa kwa viwanda vya kutengeneza mbolea pia kutasaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa ajira kwa vijana na hivyo kuongeza tija na maendeleo ya nchini. Naye Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema wizara itaendelea kusimamia taasisi zake zote zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa kilimo ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ili kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo bora kwa wakati na kwa bei nafuu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TFRA, Prof. Anthony Mshandete, alisema licha ya kuwa matumizi ya mbolea yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka, lakini matumizi hayo bado yapo chini ikilinganishwa na Azimio la Maputo la mwaka 2003 na Azimio la Abuja la mwaka 2006 ambayo yalielekeza kuongezeka kwa matumizi ya mbolea hadi kufikia kilo 50 za virutubisho kwa hekta moja. Prof. Mshandete alisema matumizi ya mbolea kwa hapa nchini yanakadiriwa kuwa ni kati ya kilo 23-25 za virutubisho kwa hekta moja na kwamba matumizi hayo madogo ya mbolea yamechangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa elimu ya juu ya umuhimu wa matumizi sahihi na faida za mbolea na bei kubwa ya mbolea itokanayo na mbolea nyingi kuagizwa nje ya nchi.



Wateja wa Benki ya Biashara ya Mwalimu (MCB), wakikata keki kwa pamoja kuadhimisha kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja jijini Dar es Salaam wikiendi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika lajengea wanafunzi kivuko

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA linalojishughulisha na kuzuia ajali barabarani nchini (AMEND) limeendelea na jitihada za uboreshaji wa miundombinu ya barabara, baada ya kujenga kivuko kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Wailes na wenye mahitaji maalum iliyopo Temeke jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika uzinduzi wa kivuko hicho jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Mkoa wa Kipolisi wa Temeke, Mrakibu Msaidizi wa Polisi Victor Ayo, alipongeza AMEND kwa jitihada za kuboresha miundombinu hiyo husus an kwa shule za msingi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum.

Alisema ubunifu huo ni mkubwa baada ya kuona kivuko cha awali hakikidhi vigezo, alisema Jeshi la Polisi litaendelea kuunga mkono jitihada za AMEND kuhakikisha wanafunzi na watu wenye mahitaji maalum kuwa na amani wanapovuka barabara.

Kamanda Ayo alitoa wito kwa madereva kutii sheria wanapofika katika vivuko hivyo (Zebra Crossing) ili kuwapa nafasi wanafunzi na watu wenye mahitaji maalum kuvuka kwa amani pale wanapohitaji kuvuka katika maeneo hayo ya vivuko.

Naye Meneja Miradi kutoka AMEND, Simon Kalolo, alisema wameshirikiana na serikali upande wa TARURA, Ofisi ya Mkurugenzi na Jeshi la Polisi kuhakikisha wanafunzi wa Shule ya Wailes na watu wenye mahitaji maalum wanapata kivuko hicho sambamba na kutoa elimu kwa madereva kuwajibika ipasavyo kufuata sheria wanapofika katika vivuko husika.

Mwenyekiti wa Usalama Barabarani Taifa kwa watu wenye ulemavu, Ditram Kabatele, alipongeza juhudi zilizofanywa na AMEND na kutaka zoezi hilo kufanyika nchi nzima.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Wailes, Jaribu Bakari, alisema ujenzi wa kivuko hicho utasaidia kwa kiasi kikubwa kwa wanafunzi wa shule hiyo kwa kuondoa adha ya kuvuka pale wanapoingia au kutoka maeneo ya shuleni.

ama
ALHAMISI OKTOBA 15, 2020
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**DK. BONIFACE: HII NDIO MOI MPYA**


Ukurasa 13

Ijue siri ya Kagera kung'ara unyonyeshaji vichanga vyake


Ukurasa 14

**Afya bora ya akili inavyoanzia katika nidhamu bora ya mtoto**

AFYA

**Na Yasmine Protace**

# Upate ukweli wa Msalaba Mwekundu, mizizi yake

MSALABA Mwekundu au Red Cross ni neno maarufu duniani na kihistoria, hasa pale panapotokea majanga mbalimbali. Hawa ni wanaojitolea kufanya kazi kuwanusuru majeruhi na misaada mingineyo.

Ni shirika la muda mrefu linalofanya kazi ya kuhudumia wanajamii au kutoa huduma ya kwanza kwa waliopata matatizo mbalimbali katika vita na majanga ya moto.

Katibu Mkuu wa Msalaba Mwekundu Tanzania, Julius Kejo, anasema asili ya mwasisi huyo ni mfanyabiashara kutoka nchini Uswisi, Herny Dunant, aliyeandika kitabu mwaka 1862 kuifahamisha dunia vita na akatoa mapendekezo ya kupunguza madhara yake.

Anasema, mzaliwa huyo wa mwaka 1822 aliyefariki mwaka 1910, kazi yake ilisaidia sana watu nchini Uswisi. Mwaka 1901, alitunukiwa zawadi ya kwanza ya Amani ya Nobeli.

Anasema vita tajwa vilitokea mwaka 1859 Kusini mwa Italia na akapendekezwa katika hilo: Kuanzishwa Shirika la Msalaba Mwekundu, ambalo ilitaka kuundwa mashirika yasiyofungamana upande wowote katika nchi.

Kejo anataja pendekezo lingine ni kuwapo mkataba wa kimataifa kulinda na kusaidia majeruhi wa kivita; na lingine kulikuwapo nembo ya kutambulika kote duniani, inayoonyesha kutofungamana na upande wowote, ikijitatambulisha na kulinda wafanyakazi wanaotibu.

Anasema matokeo ya mapendekezo ya mwaka 1863, ndio yalianzisha Kamati ya Kimataifa ya Kudumu huko Geneva, Uswisi kuhudumia majeruhi wa kivita.

Katibu huyo anasimulia kuwa, Msalaba Mwekundu ilianza kutumika kwa kuweka nembo ambayo inalinda majeruhi na wafanyakazi wa kutoa huduma za kibinadamu na mwaka 1859, Red Cross Society ilianzishwa katika nchi mbalimbali.



Mtumishi wa Shirika la Msalaba Mwekundu, akitoa msaada kwa wahitaji. **PICHA: MTANDAO**

Tanzania ilianza kabla ya Uhuru na mwaka 1949 kulishakuwapo shughuli zake nchini. Kejo anaendelea kuwa:" Mwaka 1962 ilitungwa Sheria Namba 71 ya Mwaka 1962 ambayo Red Cross ikianzishwa Tanzania.'

Anasema, imekuwa ikihamasisha kuchangia damu, ili kunusuru wenye uhitaji wa damu na asasi hiyo ni wasaidizi wa serikali, mamlaka za umma na watu wanaokabiliwa na matatizo mbalimbali ya kiafya na kijamii.

### MAJUKUMU YAKE

Kwa mujibu wa Naibu Katibu Red Cross Tanzania, John Busunga, Msalaba Mwekundu hufanya kazi ya kujitolea, akimaanisha majukumu yake kwamba:

"Huduma ya kwanza ni muhimu jamii kuijua, kwa sababu mtu anapopata tatizo, wanamsaidia na baadaye kumpeleka hospitali, kama tatizo bado litakuwapo."

Anafafanua kuwa, baadhi ya watu wanapata matatizo katika miili yao, lakini watu wanakumbana na matatizo pale wanapokosa huduma ya kwanza na kuchangia uokoaji maisha ya binadamu, kwa kutoa msaada kwenye matatizo.

Busunga anasema asilimia 80 ya shughuli za Msalaba Mwekundu zinafanywa na watu vijijini na Mhamasishaji Mkuu, Dk. Christopher Nzera, anasema zilianza kutolewa kupitia kamati za kimataifa.

Anasema kuanzishwa kwake ni kuwasaidia walioumia vitani, lengo lingine ni kustawisha haki na afya kwa binadamu, ikiwa asasi isiyobagua.

Pia, Naibu Katibu anasema wamekuwa wakiwafundisha watu namna ya kufanya huduma ya kwanza, ili iwasaidie watu penye matatizo na kuna miradi 25 nchini, wanayoiendesha nchi nzima.

Hapo anataja mradi uliokuwapo mkoani Kigoma, kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mazingira magumu, kwa kuwapa mitaji na kujifunza ufundi kama wa cherehani na makenika.

Anasema kuna mradi kwa vikundi 21 vilivyoundwa kwa ajili ya ujasiriamali; na mradi wa majisafi na salama kuzifikia kaya 5000 nchini, huko Simanjiro mkoani Arusha.

"Simanjiro kaya 3420 katika vijiji vitano, wamewasaidia shule kupata maji na vyoo," anaeleza na kuongeza kuwa wakimbizi zaidi ya 100,000 kutoka nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DCR) na Burundi, wanahudumiwa na madaktari na chumba cha mochwari.

Kuhusu huduma ya kwanza, anasema inafanyika katika mikoa yote kitaifa.

Mratibu wa Msalaba Mwekundu, Pemba, Selemani Mohamed Ally, anasema ni kosa kutumia nembo ya 'Red Cross' kwenye huduma ya dawa au kuweka katika nguo za kufanyia kazi.

Anasema msako ukianza kwa kuwakamata wanatumia nembo ya Msalaba Mwekundu, ikitumika kuitapeli mhusika anatozwa faini kati ya shilingi milioni tatu hadi tano.

AFYA

# DK. BONIFACE: HII NDIO MOI MPYA

• Asema kila kitu kupatikana hapa hapa nyumbani



Kazi ikiendelea ndani ya maabara ya MOI. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mary Geofrey**

NI jambo lililoshika kasi na kufahamika kwa wengi, nyumba ya tiba Muhimbili ilivyogawanyika katika mikondo kadhaa, zikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH); Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI); na mgeni wao Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

MOI iko mahsusi katika tiba za kibingwa kwa mgonjwa aliyevunjika kiungo cha mwili, kukiwapo tiba za mifupa aina zote, upasuaji mishipa ya fahamu na ubongo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, katika mazungumzo yake na Nipashe, anasema kuna maboresho makubwa yaliyofanywa kusaidia kuendelea kuboresha huduma za matibabu, hata kupunguza safari nje ya nchi kutafuta matibabu.

Dk. Boniface, anadokeza: "Taasisi imeokoa Sh. bilioni 48 ambazo zitatumika kwa shughuli nyingine za maendeleo ya nchi."

Anataja maeneo ya maboresho ya matibabu ya kibingwa ya mifupa, ubongo, uti mgongo na mishipa ya fahamu, yenye tafsiri ya kuokoa maisha ya Watanzania na kuokolewa pesa za serikali ambazo zingetumika kwa ajili ya tiba za nje ya nchi.

Historia yake, MOI ilianzishwa kisheria mwaka 1996 na Mkurugenzi Mtendaji Dk. Boniface, anataja kiwango cha maboresho kilichopo katika miaka mitano iliyopita, kuna ongezeko la agonjwa wa upasuaji kutoka 400 hadi 500 kwa mwezi hadi 700 kufika 900 wa hivi sasa .

Anatoa takwimu ya jumla ndani ya miaka minne, kuna wagonjwa 53,700 waliofanyiwa upasuaji kibingwa, mkurugenzi akiainisha katika mchanganuo ufuatao:

Kubadilisha nyonga 1,041; kubadilisha magoti 1,035; upasuaji mfupa wa kiuno 684; upasuaji ubongo 1,034; na watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 2,467, zote zikiwa na gharama ya Sh. bilioni 20.625, tofauti na gharama ya Sh. bilioni 68.625 iwapo wagonjwa wangepelekwa nje ya nchi.

> "Vilevile mashine hii, ina uwezo wa kutibu damu iliyoganda kwenye mishipa ya damu miguuni. Uwepo wa maabara, unaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi chache barani Afrika zinazotoa huduma hii.

**HUDUMA MPYA**

Dk. Boniface anasema kuna huduma ya upasuaji magoti na mabega kwa njia ya matundu (Athroscopy), iliwafikia wagonjwa 1,023.

Upasuaji kuondoa uvimbe wa mishipa ya damu kwenye ubongo (celebral aneurysm) imefanywa kwa wagonjwa 20 na upasuaji wa kunyoosha vibiongo kwa watoto 15; pia huduma ya upasuaji uti wa mgongo kwa kupitia tundu dogo (invansive spine surgery) wagonjwa 204.

Pia, kuna wodi mpya maalum ya kulazwa na kufanyiwa upasuaji siku hiyo hiyo (same day surgery) walinufaika wagonjwa 1,789.

Anataja huduma nyingine ni tiba ya kupata dawa za usingizi pasipo kulala (Regional Block Anaesthesia) iliyotolewa kwa wagonjwa 35 na tiba ya radiolojia (Intervention Radiology) kwa wagonjwa 18.

"Huduma hizi mpya zimeiwezesha taasisi kupunguza kwa kiasi kikubwa rufani za wagonjwa nje ya nchi. Kwa sasa kwa magonjwa ya upasuaji wa neva kwa asilimia 95 tunafanya hapa na upasuaji mifupa kwa asilimia 98 tunafanya hapa," anasema.

Dk. Boniface anasema, huduma za karakana ya viungo bandia zimezidi kuimarika kutoka 50 hadi 90 kwa mwaka hadi viungo 350 mpaka 400 vinatengenezwa kwa mwaka.

"Katika kipindi cha miaka minne tumefanikiwa kutengeneza jumla ya viungo bandia 2, 783," anasema Dk. Boniface.

**FAMASIA**

Mkurugenzi anasema maduka ya dawa yanaendelea kuboreshwa, yakitoa dawa zote muhimu kwa ufanisi asilimia 95, wameongeza madirisha ya kutoa huduma za dawa hadi kufikia nne, tofauti moja.

"Tumefungua duka la dawa la jamii (community pharmacy) hivi karibuni, kuhakikisha dawa zote zinapatikana kwa asilimia 100," anasisitiza.

**UPASUAJI UBONGO**

Dk. Boniface anasema Mei mwaka jana, serikali ilishatoa Sh. bilioni 7.9 za kujenga maabara ya kisasa kupasua ubongo, pasipo kulazimika kufungua fuvu la kichwa.

"Vilevile mashine hii, ina uwezo wa kutibu damu iliyoganda kwenye mishipa ya damu miguuni. Uwepo wa maabara, unaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi chache barani Afrika zinazotoa huduma hii," anasema.

**TIBA MTANDAO**

Kitaalamu inaitwa telemedicine na MOI imejenga chumba maalum cha madaktari katika sehemu mbalimbali nchini, wanaotumia picha za X-Ray na CT-Scan, zinazosomwa na madaktari bingwa wa radiolojia wa MOI na majibu yanarudishwa kwa daktari aliyeomba, ndani ya muda mfupi.

Anasema huduma hiyo tayari imeshaunganishwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

**UWEKEZAJI MIUNDOMBINU**

Dk. Boniface anasema serikali ilishatoa Sh. bilioni 16.5 za kukamilisha mradi wa jengo jipya la MOI na kununua vifaa tiba vya kisasa.

Anasema vitanda vimeongezeka kutoka 150 hadi 362 na hakuna mgonjwa anayelala chini, pia vitanda vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (intensive care unit) vimeongezeka kutoka vinane hadi 18.

Kingine anakitaja ni kinachoitwa 'High Dependency Unit' (kitengo cha utegemezi wa hali ya juu), kilichopatiwa vitanda 16.

Vyumba vya upasuaji ndani ya miaka hiyo minne, imeongezeka kutoka sita hadi tisa na kuongeza chumba kikubwa cha kisasa cha maabara na cha vipimo vya radiolojia.

Vivyo hivyo, vyumba vya wenye hadhi maalum (executive rooms) na kufika 32; chumba maalum cha kufanya upasuaji bila kulazimika kulala hospitali (Same Day Surgery) na chumba kikubwa cha mapokezi ya dharura, maarufu "emergency room"

**VIFAA TIBA**

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, anasema imenunua mashine za kisasa za radiolojia; MRI, CT-Scan, Digital X-ray, CR X-ray, Portable X-Ray, Ultrasound 2 na C-arm.

Kwa mujibu wa Dk. Boniface, taasisi imeshanunua mashine sita za kutoa dawa za usingizi (anaesthesia machines); vifaa vya ICU na HDU vikiwamo vitanda vya kisasa (monitors na ventilators).

Taasisi imenunua vitanda vya upasuaji sita na Microscope ya kisasa kwa ajili ya upasuaji ubongo na uti wa mgongo; ununuzi wa mshine mbili mpya za kisasa za vipimo vya maabara.

Orodha ya mkurugenzi ina vifaa vipya vya kisasa vya mazoezi tiba (physiotherapy); mashine ya kupooza hewa kwenye vyumba vya upasuaji (chiller); na mashine ya kuchoma taka.

**HUDUMA UMMA**

Dk. Boniface anasema, MOI imeshaingia mkataba na Hospitali ya Nyangao, Lindi kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi mikoa ya kusini.

Pia, anasema katika kipindi cha mwaka mmoja sasa, madaktari bingwa wa MOI wamewahudumia wagonjwa wa nje 925 katika kliniki za kawaida na kuwafanyia upasuaji mkubwa zaidi ya wagonjwa 528.

"Taasisi ina mpango wa kuanzisha ushirikiano huu na hospitali nyingine za mikoa na kanda hapa nchini ili kusogeza huduma zetu kwa wananchi," anasema Dk. Boniface.

Anasema hivi sasa wanaendeleza ushirikiano mzuri na taasisi za kimataifa kufanya kambi za upasuaji wa wagonjwa, mafunzo kwa wataalamu wake na tafiti za misaada ya vifaa tiba. Kwa mujibu wa Dk. Boniface, MOI iliingia mkataba wa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Peking, China kuendeleza fani ya upasuaji ubongo na mishipa ya fahamu.

Anasema timu ya kwanza ya wataalamu kutoka Beijing walikuja, MOI Februari mwaka jana na wataalamu wa tano, MOI walihudhuria mafunzo ya miezi mitatu ya Chuo Kikuu cha Peking.

Eneo lingine ni Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Tiba Muhimbili (MUHAS), taasisi imeendelea kufundisha wataalamu wa mifupa, mishipa ya fahamu na upasuaji ubongo.

Vilevile anataja taasisi imeendelea kuwa hospitali ya kufundisha madaktari kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika.

AFYA

# Ijue siri ya Kagera kung'ara unyonyeshaji vichanga vyake

• Wazee wao nao wana ya kwao

Na Jaliwason Jasson, Bukoba

JAMII inapaswa kutafakari hiari ya unyonyeshaji watoto bila lishe mbadala ndani ya miezi sita. Hata hivyo inaelezwa hilo limeshindikana kutekelezwa vyema.

Mkoa wa Kagera una rekodi inayokinzana na hilo, kwani unang'ara katika unyonyeshaji watoto, kuanzia wanapozaliwa hadi umri miezi sita ya awali.

### WATAALAMU LISHE

Takwimu za mwaka 2018 zinataja asilimia 96 ya watoto wanaonyonya ndani ya saa moja ni asilimia 97 na wananyonya kwa miezi sita ni asilimia 86, huku walionyonya kwa miaka miwili ni asilimia 44.

Mtaalamu lishe anayejitambulisha kwa jina Hamis, anasema mbinu wanayoitumia ni utoaji elimu kupitia vyombo vya habari vya kijamii na kitaifa, kuifunza umma ubadilike, ili mkoa upige hatua katika unyonyeshaji.

Kiongozi huyo anataja mbinu nyingine, wahudumu wa afya ngazi ya jamii hupeleka elimu kwa walengwa kinamama wanaonyonyesha na wajawazito na kuhakikisha vituo vya afya vinavyotoa huduma vina wataalamu wanaosaidia elimu ya unyonyeshaji kwa kipindi hicho wajawazito wanapohudhuria kliniki.

Aidha, Hamis anasema kuna mikataba kati yao na maofisa watendaji kata, vijiji na mitaa wanaokuhakikisha kila mama uhudhuria kliniki, anapata elimu ya unyonyeshaji na namna ya kuandaa chakula lishe.

Kimsingi, ni mkakati wa mabadiliko chanya unaochangia mkoa kufanya vizuri kwa watoto wenye umri chini ya miezi sita na waliovuka.

"Tunaangalia kijiji ambacho kina hali mbaya na tunawapa vipimo na kuwapa elimu wazazi na watoto," anaeleza Hamis, akisema wanafuatilia kila baada ya muda uliotengwa kama vile miezi sita na mwaka, kuona namna ya kuwasaidia wahusika.

Mtaalamu huyo anasema unyonyeshaji ni suala la kisaikolojia na linatakiwa kuwekewa mazingira rafiki kwa mama ili kuepuka dai 'maziwa hayatoki.'

### MAZIWA YALIVYO

"Mtoto anapokuwa ananyonya ile sehemu ya titi nyeusi iwe ndani kwenye mdomo wa mtoto na mtoto asishike lile titi na tumbo la mama na la mtoto vigusane, ili apate lile joto la mama ...mtoto akamate vizuri titi."

Anafafanua kuwa, mtoto anapokamata vizuri titi, kuna sauti itasikika, lakini asipokamata anaangukia kulia na ndio anaanza kumng'ata mama yake.

Hamis anasema maziwa ya mama yamegawanyika katika sehemu kuu mbili; maji na maziwa na mama anaponyonyesha anatakiwa amuweke mtoto kwenye titi moja mpaka ashibe, kwani kumbadilisha titi kunamfanya anyonye maji na siyo maziwa.

Anasema, mtoto anatakiwa anyonye kwa dakika 20 hadi dakika 30, huku mama asiwe anafanya suala jingine na mtoto anapomng'ata mama, ni ishara hapati maziwa vizuri na anatakiwa anyonye kadri anavyohitaji, asipangiwe usiku muda wa kunyonyesha.

Mtaalamu huyo anapinga unyonyeshaji wa mazoea. Mtoto anaponyonya anatakiwa ama kuimbiwa au kucheza ili kumpa furaha na kuufanya ubongo uchangamke kwa ajili ya kufanya utambuzi wa vitu mbalimbali.

Anashauri mama wanaonyonyesha kula makundi kadhaa ya vyakula akivitaja vyakula vya nafaka kama mahindi, mchele, mtama na ndizi mbichi; kundi jingine ni protini kama vile maharage, soya, maziwa, samaki na nyama.

Makundi mengine ni mboga, matunda kama ndizi mbivu, maembe, papai, parachichi, pasheni; pia mwisho ni sukari mafuta na asali.

### WAZAZI WANYONYESHAJI

Nyangoma Busenene mkazi wa Kashai, anasema suala la kumnyonyesha mtoto ni baraka kwao na linakuza kiumbe, akitaja utamaduni wao unatilia maanani vyakula vinavyohoshauriwa kitaalamu na wazazi.

Busenene anasema vyakula hivyo ni vya kawaida na vinapatikana kwa gharama katika mazingira yao, akitaja mfano wa jamii ya nyanya chungu.

Mkazi wa Katoma, Asha Mussa, anasema kinachowasaidia katika unyonyeshaji bora ni kufuata ushauri wa wataalamu wa afya na lishe kliniki na mafunzo ya wazazi wao.

Kwa mujibu wa Asha, elimu hiyo ni ya kurithishana vizazi, hivyo anayekiuka kwa makusudi haivumiliwi kijamii kwa ajili ya ustawi wa mtoto.

Mkazi wa Kastamu, Juster Rweyemamu, anaona chanzo cha mafanikio unyonyeshaji wa miezi sita mfululizo inatokana na mkoa huo kuwa na uhakika wa chakula.

Juster, anataja ukaribu na Ziwa Victoria kunawapa lishe, pia mifugo ya kutosha nayo inawasaidia uhakika wa lishe hata kumudu unyoyeshaji.

Mkazi wa Kyakailabwa, Martha Bwenge, mwenye umri miaka 79, anakumbusha unyonyesha hauhitaji uzembe, kwani ndiko kwenye msisitizo wa wataalamu wa lishe na afya.

Bibi huyo anaungana na siri ya mafanikio ya mkoa wa Kagera, ni mila na desturi zikiwamo babu na bibi kuwaridhia watoto kukaa, hata katika hatua ya kuacha ziwa, mtoto anapokabidhiwa asubuhi mapema.

"Babu yake huwa anauliza kama mama yake mjamzito hapo ndio anaweza kukubali mtoto aachishwe na umri uwe unaruhusu, lakini kama umri wake ni mdogo na mama hana matatizo ya kiafya anaambiwa asimwachishe," anasema Bwenge.

Aidha, anasema sheria ndogo za ukoo wanazojiwekea zimesaidia kuepuka ukiukaji maadili, hata kushindwa kuwanyonyesha watoto kwa kipindi cha miezi sita bila kumpa chochote.

George Mulokozi anachangia kinachosaidia ni kutii kanuni afya, kujua na kuheshimu wajibu wa kumtunza mtoto, baba na mama wakisimamia kikamilifu unyonyeshaji wa miezi sita ya awali, pia kwa mtoto siku ya kwanza.

Frank Byamungu, anahusisha uzembe katika unyonyeshaji unaweza kuwagharimu wazazi wote wawili.

### MIKAKATI GANI?

Nipashe ilidokezwa, Kamati ya Lishe Mkoa Kagera, hufanya vikao kila baadaye ya robo mwaka, chini ya uenyekiti wa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), wakiwa na mkakati wa bajeti kumtengea Sh. 1,000 kwa kila mtoto.

Pia, wanashirikiana na wadau kufanya urutubishaji wa vyakula vya lishe hasa unga wa lishe ambao utakuwa na mchanganyiko wa makundi yote vyakula.

Mratibu wa Huduma ya Mzazi na Mtoto Mkoa wa Kagera Neema Kyamba, anasema elimu ya unyonyeshaji kwa miezi sita ya kwanza, huwa wanawapatia wanawake wakiwa wajawazito na baada ya kujifungua ndani ya saa moja wanatakiwa kunyonyesha.

Aidha, anahimiza mama kumnyonyesha maziwa yake pekee, yakibeba mlo kamili na mtoto akiwa anaponyonya vizuri, hakuna haja kumpa kingine maana hakiongezwi chochote. Mratibu huyo anataja athari za kumnyima kunyonya ni kupata majipu, usaha na homa.

Anafafanua: "Na mama usipomnyonyesha mtoto unapata ujauzito kwa kuwa kunyonyesha ni njia ya asili ya uzazi wa mpango.

"Kunyonyesha kunajenga ukaribu na upendo unakuwapo mfano unapolala naye unasikia moyo wa mtoto unadunda," anasema.

Vilevile anasema, mtoto anaponyonya vizuri, unamfanya mama yake anaoisikia tumbo linauma kutokana na kurudi kizazi, lakini inaweza ikatulizwa na nyonyo.

### WADAU

Mratibu wa Shirika la Kikukwe Community Development Initiatives (KCDI), Christine Nyangoma, anaungana na wataalamu akiwa na hoja ya kitaalamu wazazi wenye umri miaka 25 hadi 35 wananyonyesha katika namna isiyo sahihi wakiona ni ya kisasa, akiibatiza jina 'kidotcom.'

Anatoa mfano wa mzazi anayenyonyesha, huku akipiga simu, jambo ambalo si sahihi.

Nyangoma, anayefanya kazi wilayani Misenyi, Tarafa ya Kiziba, anachangia kilichoinua mkoa wa Kagera, kung'ara katika unyonyeshaji watoto wachanga katika miezi sita ya awali ni ukiitwa 'Mradi wa Mtoto Mwerevu' ulioanzia Misenyi mwaka 2015, sasa huko ngazi ya mkoa.

Anasema mnamo Oktoba 2017 walikuwa na walengwa watoto 10,000 katika siku 1000 walizojitengea, yaani miaka miwili na miezi tisa, walikofikia mafanikio asilimia 86.2 mwaka 2018 na kitaifa asilimia 58.1.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria duniani asilimia 40 ya watoto wachanga chini ya umri wa miezi sita ndio wanaonyonyeshwa pekee, sababu zinazotolewa juu ya kasoro hiyo ni kazi, magonjwa na utamaduni.

Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), katika ripoti ya utafiti, watoto na vijana wadogo walionyonyeshwa wakiwa wachanga wana uwezekano mdogo wa kupungua uzito mwilini kupindukia.



Kinamama mkoani Kagera, wakiwa katika shughuli inayohusisha unyonyeshaji. **PICHA: MTANDAO**

> **"Mnamo Oktoba 2017 walikuwa na walengwa watoto 10,000 katika siku 1000 walizojitengea, yaani miaka miwili na miezi tisa, walikofikia mafanikio asilimia 86.2 mwaka 2018 na kitaifa asilimia 58.1.**

AFYA

MALEZI YA MTOTO

# Afya bora ya akili inavyoanzia katika nidhamu bora ya mtoto

• Aliyeshindikana nyumbani, ashangaza shuleni

**Na Martha Mwasyeba**

KUNA mwalimu mmoja maarufu nchini Marekani, Bill Graham alishawahi kutoa wosia wake kwamba: "Urithi pekee ambao mzazi anaweza kumwachia mtoto wake au wajukuu zake sio fedha wala mali zote ambazo amechuma kipindi chote cha uhai wake, bali ni kumwachia tabia nzuri na imani".

Pia mwimbaji wa muziki, Stacia Tauscher alishawahi kutamka: "Tunatumia muda mwingi kuwaza kesho ya watoto wetu bila kuwaza leo yao."

Hivi sasa wazazi wengi wanatumia muda mwingi kuwaza kuweka malengo ya watoto wao kufika vyuo vikuu na maisha yao bora ya baadaye, wakisahau kwamba kupanda mbegu bora leo ndiyo inatoa matunda ya hapo baadaye ambayo, ni tabia njema.

### WASOMI WANAVYOLIOA

Hilo linaporudi katika taaluma, mwanazuoni JTY Hunt wa Chuo Kikuu wa North Carolina Marekani, miaka 68 iliyopita alifafanua dhana nidhamu ni afya ya akili inayoegemea kufanya uamuzi sahihi, baada ya kutafakari, huku mhusika akichukua tahadhari sahihi, kabla ya kuitenda.

Kwa sasa kuna wengi wanashuhudiwa katika hisia za 'wazazi bora' kwa watoto wao kutokana na wanayowatendea watoto wao, jambo ambalo katika uhalisia ni virusi sumu kwa taifa lijalo, vijana wakishuhudiwa tabia mbaya, mzizi mkuu ni malezi kutoka majumbani.

Mwandishi wa vitabu, Myles Munroe, alishadokeza katika andiko kwamba: "Ndoto ni sawa na 'diski' tupu ndogo inayotegemea wewe unataka kuweka kitu gani ndani yake kutokana na mtu unavyopenda kusikia kutoka katika hiyo 'diski' ndogo.

"Sasa ajabu ni kwamba wengi wetu tumeweka vitu katika 'diski' hiyo, lakini hatutaki kusikiliza au kuona vile tulivyoweka sisi wenyewe."

Hapo ndipo kilichomo katika methali 'utavuna unachopanda.' Ni kawaida kizazi kilichopo kubarikiwa wasomi wenye vyeti bora, lakini wanakosa matunda ya kazi zao na umuhimu jamii, bali. Shida kuu inatajwa kuwa tabia.

Kimantiki, inatajwa ni vibaya kuelemea sura moja ya malezi, ambayo ni elimu ya makaratasi na kusahau hitaji la elimu ya wazazi, ambayo ina nafasi kubwa.

Swali linalowaangukia wazazi, kulikoni mtoto (kwa baadhi ni mmoja), anashindakanaje kulelewa kwa misingi stahiki nyumbani, lakini anapopelekwa shuleni kwenye kundi kubwa la wenzake panawezekana, ilhali mzazi huyo anamjua kwa kina? Hapo kuna kasoro inayoibuliwa.



Namna ulivyo urafiki na nidhamu kati ya mtoto na mzazi au mlezi. **PICHA: MTANDAO.**

> Sasa ajabu ni kwamba wengi wetu tumeweka vitu katika 'diski' hiyo, lakini hatutaki kusikiliza au kuona vile tulivyoweka sisi wenyewe.

### SHIDA ILIKO

Hivi sasa kuna mtazamo wa kuwapo wazazi wanaoiga malezi yanayoshudiwa kutoka mbali, kupitia mifumo ya utandawazi iwe vyombo vya habari au mifumo mingine ya mawasiliano ya umma, pasipo kujiwekea dira ya manufaa na hasara ya badaye.

Hapo imechangia kwa baadhi ya wazazi walioshuhudia zama zilizopita, ni kwanini hawaigi mfumo wa ulezi kipindi kilichopita na manufaa yake yanayodumu hadi kipindi kilichoko? Kuna waonathubutu kuyabebesha tafsiri 'hayana maana hata kidogo.'

Uzoefu wa utamaduni wa malezi katika kipindi kilichopita unajihidhihirisha katika nidhamu iliyokuwapo, ambayo ni kipengele cha afya ya jamii. Kilichojiri wakati huo, kinakinzana na kilichopo sasa.

Ndani ya zama zilizopita binti alikuwa "wa jamii nzima" wakati sasa wameshabadilika kuwa "wa wazazi wake tu" jambo linalowafanya wazazi kutokuwa tena na uchungu kwa watoto wa wenzao.

Dhana hiyo inazaa simulizi ya mwanamama anayebeba simulizi yenye malalamiko namna mwanawe alivyokuwa na simulizi ya matikio ya wizi, mama huyo akikutana nayo kila alivyorejea nyumbani kutoka kazini.

Mama huyo anayelalamika anatoa ushahidi wa matukio, vitu anavyotuhumiwa kuiba, zikiwamo baiskeli za wenzake, zilipatikana kwenye uvugu wa kitanda.

Suluhisho la mama huyo, analitaja kumpeleka mtoto katika shule tofauti kumjengea mazingira mapya. Alishangaa kuona mtoto ana mabadiliko ya kitabia yanayoangukia maadili mema.

Hapo ndipo mama huyo akaangukiwa na swali binafsi: "Je, walimu wamefanya nini kugeuza tabia za mtoto huyu nami nilishindwa nini?"

Hapo ndipo ukaibuka majibu ya mzizi wa mageuzi tajwa, mzazi alimpenda sana, huku akishtuliwa sana na makosa yake, lakini alishindwa kuyafanyia uamuzi sahihi, kama vile kumpatia adhabu stahiki.

Ni aina ya mtazamo unaoanika tabia ya wazazi wanajali sana ufaulu masomoni, baadhi wakiangukia imani ya kumudu lugha ya Kiingereza, kuliko maisha halisi yanayomzunguka katika jamii.

Pia, kunatajwa tabia ya wazazi kuoegea mengi yasiyotahiki mbele ya watoto wenye umri mdogo na matokeo yake ndio kuiga mtazamo wenye athari kwa watoto.

Kuna mkasa wa mtoto mwenye umri miaka tisa aliomba simu kwa mgeni wao, achezee simu, haikuchukua dakika nyingi alifunga ule mchezo na akahamia upande wa meseji, akizisoma moja hadi nyingine.

Mwenye simu alijiuliza mtoto huyo anafanya uchunguzi gani? Baadaye aligundua, kuna vitu wazazi wake wanaongea mbele ya mtoto, ambaye sasa anataka kuvihakiki. Ni tabia wanayojifunza vijana hao walioharibikiwa nidhamu.

Wazazi wengi wamekuwa watu wa kuchukulia mtoto mabaya hayo ya kawaida, bila kujua kuna mipaka ya kukagua mtoto huyo, kwa umakini ili kutoharibu kizazi chetu kinachokuja, kwa namna ya kipekee nafasi ya televisheni na katuni zinapaswa kuangaliwa.

Kwa asili, mtoto huwa anaishi maisha ya wazazi, wataalamu wa saikolojia wakisema kwamba asilimia 80 ya mtoto anajifunza kwa kuona, kuliko kusikia.

Maana yake nini? Maisha ya wazazi yanaposheni ugomvi, matusi na kutoelewana, ndicho kinachopandikizwa katika katika maisha ya watoto. Hivyo, mabomu yanayotengenezwa, matarajio yake ni mlipuko wa mabomu katika maisha ndani ya muda usiotarajiwa.

Hilo linawafanya wazazi kuwa mfano wa kuigwa, mbele ya watoto wao, hata alaumiwe baadaye kwa sababu ya uharibifu unaotokea katika maisha ya watoto wao.

Kuwapo malezi bora, kunaipunguzia serikali mzigo wa wasio na nidhamu katika umma, mathalani wavuta bangi, majambazi, vibaka, wauzaji na watumiaji dawa za kulevya.

Watoto waliowasomesha kwa gharama kubwa, mara zote wanapaswa kufurahia katika mafanikio yao, ili kuwarudisha katika mstari ulionyooka.



# Mawakala benki, watoa huduma za fedha kwa simu kupewa elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA), kimeanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya mawakala wa benki na wanaoendesha huduma za fedha kwa njia ya simu kutokana na sekta hizo kukua kwa kasi nchini.

Aidha, chuo hicho kinatarajia kufungua tawi lake jijini Dodoma mwishoni mwa mwaka huu kwa ngazi ya shahada ya uzamivu na mafunzo hayo ya muda wa wiki sita.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema mafunzo hayo yanalenga kuchochea masuala ya kiuchumi ili kuwapo na uchumi shirikishi wenye weledi na ujuzi.

Alibainisha kuwa katika Mpango Mkuu wa Maendeleo Sekta ya Fedha nchini wa miaka 10, taasisi za elimu ya juu nchini na taasisi za utafiti zimeagizwa kutumia fursa zilizo kwenye mpango huo, ili kujipanga katika kuboresha maeneo ya kitaalamu na kiutafiti ili sekta iendelee kukua na kuhimili ushindani na mabadiliko.

“Kwenye mpango kuna maagizo kwenye taasisi za elimu ili kufanikisha kufikia malengo hayo, tukaamua kuanzisha kozi za muda mfupi ambazo zitakuwa za wiki sita kwa Agent Banking na Mobile Money kutokana na sekta hii ndio inaonekana kukua kwa kasi lakini watoa huduma hawana utaalamu huo,” alisema.

Alisema sekta hiyo inakuwa kutokana na uwekezaji wa serikali kwenye masuala ya mawasiliano na upatikanaji wa umeme ambapo huduma hizo zipo hadi maeneo ya vijijini hivyo mafunzo hayo yatakuwa ya muhimu kwao kuwa wabobezi kwenye utoaji wa huduma hiyo.

“Ili kuendana na jitihada za serikali tumejipanga kutoa mafunzo haya ambayo yatawafikia moja kwa moja Watanzania, hii sekta ndogo ya fedha sio ndogo kama tunavyofikiri ndio eneo ambalo Watanzania wengi kwa sasa wanatumia, tunaamini hatua hii itasaidia kutambua biashara hiyo lakini kujua namna ya kuiendesha,” alisema.

Alieleza kuwa mafunzo hayo kwa sasa yatatolewa Arusha, Dar es Salaam na Dodoma na baadaye yataenda kwenye maeneo mengine.

Akizungumzia kuhusu kuanzisha tawi la Dodoma, Prof. Sedoyeka alisema wamejipanga kuanza ujenzi wa majengo yao kwenye eneo la Njedengwa Januari mwakani kwa kutumia utaratibu wa ‘force account’ ili kuanza kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya astashahada.

Hata hivyo, alisema kutokana na nusu ya wanafunzi wa shahada ya uzamivu kuwapo Dodoma wamelazimika kutafuta jengo la kukodi kwa muda ambalo litatumika kufundishia wanafunzi hao pamoja na wa mafunzo hayo ya muda mfupi.




Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, Ahadi Sinene (kushoto), akimnadi mgombea udiwani Kata ya Mbambala, Paskazia Mayala kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# UVCCM: JPM amemwenzi Mwl. Nyerere kwa vitendo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umesema Rais John Magufuli ni miongoni mwa watu wachache waliofanikiwa kumwenzi Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere kwa vitendo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, kuhusu Kumbukumbu ya miaka 21 ya kifo cha Mwalimu Nyerere, Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Kheri James, alisema Rais Magufuli amemwenzi kwa vitendo kutokana na uzalendo wake, misimamo na kuwa na maono kama ya Baba wa Taifa.

Alisema Mwalimu Nyerere alikuwa na maono ya kujenga Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mara ambapo ujenzi ulianza mwaka 1977 na haukukamilika lakini chini ya Magufuli ndoto hiyo imetimia kwa kutoa Sh. bilioni 15 ili kumalizia ujenzi huo.

Aidha, alisema Mwalimu Nyerere alikuwa na kiu ya kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma, utoaji wa elimu bure na utekelezaji wa mradi wa Bonde la Mto Rufiji wenye uwezo wa kuzalisha umeme megawati 2,100 ambavyo vyote vimefanywa chini Rais Magufuli.

Kutokana na hayo, aliwataka Watanzania Oktoba 28 mwaka huu kuwachagua viongozi wanaotokana na CCM ili waendeleze kwa vitendo mambo yaliyoasisiwa na Mwalimu Nyerere.

“Ni miaka 21 tangu ameondoka tunaendelea kutafakari uzalendo wake, utumishi wake umakini wake, msimamo wake ambapo umejenga Taifa lenye umoja na mshikamano, na aliamini rasilimali tulizo nazo zitaleta faida siku moja kwa Watanzania wote,” alisema.

Alieleza kuwa Rais Magufuli ana thamini mchango wa waliomtangulia na ana dhamira ya kweli kwa Watanzania.

“Ametuingiza kwenye uchaguzi tukiwa hatutegemei fedha za wafadhili kwa mara ya kwanza tumeingia na fedha zetu za walipa kodi, ni hatua nzuri ya kuwa na demokrasia ambayo haigharamiwi na mtu bali inagharamiwa na Watanzania wenyewe,” alisema. Alisema Tanzania ni nchi huru hivyo haitaraji uchaguzi wake kuingiliwa na mataifa mengine kama ambavyo haiwaingilii wengine.

# Serikali yaelekeza migogoro mabonde ya maji kukomeshwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewaagiza wakurugenzi wa mabonde ya maji nchini kuhakikisha wanamaliza migogoro ya maeneo hayo ili kuruhusu wananchi kufanya shughuli za maendeleo kupitia maji yaliyopo kwenye maeneo hayo.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya uwekajI saini ya makubaliano ya utendaji kazi baina ya bodi za maji za mabonde na wizara hiyo kwa mwaka 2020/2021.

Sanga alisema migogoro mingi husababishwa na watu kukosa fedha, kwa hiyo wakirekebisha migogoro wakazi wa maeneo hayo watapata fedha kutokana na maji yaliyomo kwenye mabonde hayo.

Alifafanua kuwa sheria ya usimamizi wa rasilimali za maji imezipatia bodi za maji za mabonde jukumu la usimamizi wa rasilimali za maji jambo ambalo wanapaswa kulisimamia kikamilifu.

Alisema, wizara imekuwa ikiwawezesha fedha ili kutekeleza miradi pamoja na majukumu ya usimamizi wa rasilimali za maji pamoja na kuwapatia

vifaa vya kutendea kazi kama vile magari, ofisi na kuajiri watumishi.

“Pamoja na bodi kutekeleza majukumu yake, lakini hakukuwa na mfumo mzuri wa ufuatiliaji wa utendaji kazi ambao ungesaidia kuweka mfumo wa utendaji wa bodi za maji za mabonde,” alisema Sanga.

Aidha, katibu mkuu huyo, alimpongeza Mkurugenzi wa Rasilimali za Bodi za Maji, kutokana na kukubali kusaini utaratibu wa utendaji wa kazi kwa mwaka ambapo ni fursa nzuri ya kupima utekelezaji wa malengo yaliyowekwa.

Alisema lengo la kusaini makubaliano hayo ni kupima uwepo wa utendaji kazi wa umakini katika maeneo mbalimbali ambayo kuna mabonde. Alisema mkutano huo ambao umehusisha mabonde tisa ya maji, tathmini ilifanyika kwa njia ya usaili, ukaguzi wa taarifa na kutembelea maeneo mbalimbali yaliyofanyiwa kazi.

Naye Mkurugenzi wa Bodi ya Idara za Rasilimali za Maji, Dk. George Lugomela, alisema mabonde haya yanapaswa kufanyiwa kazi vizuri ikiwamo kutangazwa ili jamii ijue. Alisema kutokana na makubaliano ambayo wamefanya watajitahidi kuhakikisha wanayatendea haki mabonde katika utendaji kazi, ili yalete matokeo chanya, kama walivyokubaliana wakati wa kusaini makubaliano hayo.

“Tutayatendea haki haya makubaliano, hivyo jamii itegemee matokeo chanya kutoka bodi za mabonde,” alisema Dk. Lugomela.





# Jaji ahimiza weledi, utendaji haki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATENDAJI wa Mahakama mkoani Mbeya wameagizwa kuzingatia weledi wa sheria katika kuwahudumia wananchi ikiwamo utoaji wa haki ambazo si kandamizi ili wananchi waufurahie mhimili huo muhimu wa kutoa haki.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Dk. John Utamwa, wakati wa ufunguzi wa jengo la Mahakama ya Mwanzo Uyole jijini Mbeya ambalo limejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 448.

Jengo la awali la mahakama hiyo liliungua moto mwaka 2018 na kuteketeza mali zote, zikiwamo nyaraka na samani huku chanzo cha moto huo kikiwa hakijulikani mpaka sasa.

Dk. Utamwa alisema uamuzi unaofanywa na baadhi ya watendaji wa mahakama huwa unasababisha uhusiano mbaya kati ya mhimili huo na wananchi na matokeo yake kuwapo uvunjifu wa amani.

"Jengo la awali la mahakama hii lilichomwa moto mwaka 2018, chanzo cha tukio hilo la moto huwa kinanipa shaka sana. Huenda lilisababishwa ama na uhusiano mbovu au uendeshaji mbovu wa mashauri. Nawaomba mzingatie weledi kwenye kazi zenu," alisema Dk. Utamwa.

Aidha, aliwaomba wananchi wanaohudumiwa na mahakama hiyo kushiriki katika ulinzi wa miundombinu ya mahakama na taasisi zingine za umma.

Jaji Utamwa aliutaka uongozi wa mahakama hiyo kufikiria namna ya kuongeza ulinzi wa jengo hilo ikiwa ni pamoja na kujenga uzio kuzunguka jengo hilo ili wahalifu wasiingie kirahisi.

Naye Ofisa Utumishi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Rajabu Singana, alisema mahakama hiyo inahudumia kata 14 za Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kwamba baada ya kuungua, kesi nyingi zilikwama.

Alisema jengo hilo liliungua Agosti, 2018 na kusababisha upotevu wa majalada ya mashauri 656 ya kesi ambazo zilikuwa zinaendelea kusikilizwa.

Singana alisema taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi mkoani hapa baada ya jengo hilo kuungua, ilibainisha kuwa lilichomwa na wananchi waliokuwa wanakabiliwa na kesi kwenye mahakama hiyo.

Kwa upande wake, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Mbeya, Denis Luwungo, alisema ujenzi wa mahakama hiyo utawezesha zaidi ya kesi mpya 552 kuendelea kusikilizwa na kwamba kati ya kesi hizo 27 ni za ndoa na talaka.



Mgombea mwenza wa urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akiwanadi wagombea udiwani wa kata mbalimbali za Jiji la Mbeya katika mkutano wa kampeni kwenye uwanja wa Shule ya Msingi Nzovwe hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mgombea ajinasibu kuibua mipango mingi ya maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mbeya Vijijini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Oran Njeza, amesema serikali iliyoko madarakani, bado ina mipango mingi na mizuri ya maendeleo kwa wakazi wa jimbo hilo.

Kutokana na mipango hiyo, amewaomba waendelee kuchagua wagombea kutoka CCM kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu, ili mipango hiyo itekelezeke.

Akizungumza kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika katika kata ya Ikukwa, Njeza alisema endapo wagombea wa CCM kuanzia madiwani, mbunge na Rais watachaguliwa, kuna miradi kedekede ambayo itafanyika ndani ya miaka mitano ndani ya jimbo.

"Kuna miradi mingi ya maendeleo kwenye jimbo letu imewekwa kwenye Ilani ya CCM ili tuitekeleze ndani ya miaka mitano ijayo, hivyo wananchi msije mkafanya makosa kuchagua wagombea wa vyama vingine kwani mkiwaacha wagombea wa CCM mtakuwa mmefifisha mipango hiyo," alisema Njeza.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni kukamilisha usambazaji umeme kwenye vijiji na vitongoji vyote, kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati na pia kujenga barabara nyingi ndani ya jimbo na baadhi yake zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Njeza aliwataka wakazi hao wa kata ya Ikukwa kuanza kujenga nyumba za waganga na wauguzi kwenye kituo cha afya, ili itakapopandishwa hadhi na kuwa hospitali, kusiwe na kero ya ukosefu wa nyumba hizo.

Naye mgombea udiwani katika kata ya Ikukwa, Petro Swila, alisema endapo atachaguliwa, ataanzisha mara moja ujenzi wa nyumba za wauguzi kwenye kituo hicho cha afya kwa kuchangia tripu 50 za mchanga.

Swila alisema kuwa anatambua kwamba kero kubwa ya wakazi wa kata hiyo ni ubovu wa barabara na akaahidi kuwa akichaguliwa kwa mara nyingine atahakikisha barabara zote zinazoingia na kutoka ndani ya kata hiyo zinajengwa.

"Natambua kuwa kero yetu kubwa sisi wananchi wa kata ya Ikukwa ni barabara. Mkinichagua hilo litakuwa kipaumbele changu, nitahakikisha barabara zetu zote zinajengwa na kuwa bora zaidi ya ilivyo hivi sasa," alisema Swila.

## Mvua yaathiri mavuno tumbaku

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

CHAMA Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya mkoani Mbeya (CHUTCU), kimesema msimu wa kilimo uliopita hali ya uzalishaji ulishuka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa hasa mvua kunyesha kupita kiasi.

Meneja Mkuu wa CHUTCU, Juma Mohamed, alisema juzi kuwa asilimia kubwa ya tumbaku iliyozalishwa ilikosa ubora kutokana na mvua nyingi iliyonyesha, hivyo kusababisha wananchi kushindwa kuanika zao hilo kwa ufasaha.

Alisema katika msimu wa kilimo wa 2018/19 mahitaji yalikuwa kuzalisha tani milioni 9.92, lakini uzalishaji ulipungua na kufikia tani milioni sita.

"Msimu uliopita wakulima walipata hasara kubwa sana kwa sababu walitumia gharama kubwa kuzalisha hususan ununuzi wa pembejeo za kilimo kama mbolea ambazo zilisombwa na maji na wengine waliovuna walishindwa kuanika," alisema Mohamed.

Aidha, alisema kuwa kwa kipindi hicho bei ya tumbaku ilipungua kutoka Dola 1.6 mpaka Dola 1.33 na kwamba hali hiyo ilitokana na tatizo la kupungua ubora na uzito wa tumbaku hususan kushuka kwa soko.

Mohamed alisema kutokana na tatizo hilo kwa msimu huu wa kilimo tayari wamefanya maandalizi ya kimkakati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo hasa mbolea na mbegu.

Alisema pembejeo na mbegu walizoandaa msimu huu zitawafikia wakulima 7,500 walio katika vyama vya msingi vya ushirika 23 vilivyomo wilayani humo.

Baadhi ya wakulima wa tumbaku wilayani hapa waliiomba serikali kuwasaidia kupatikana kwa soko la uhakika ili wanufaike na zao hilo kwa maelezo kuwa msimu uliopita walipata fedha ambazo ziliwasaidia kulipa madeni na hawakupata faida.

Mmoja wa wakulima hao, Salome Kilasi, aliomba wafikiwe na pembejeo mapema ili kuepuka mawakala wa pembejeo ambao huwa wanawasambazia pembejeo feki ambazo zinawasababishia hasara kwenye kilimo.

Aliomba pia wataalamu wa kilimo kwenye halmashauri wahimizwe kwenda mashambani kwa wakulima kuibua matatizo yanayowakabili wakulima na kuyatafutia ufumbuzi mapema.

# Maalim Seif atamba CCM haina chake kisiwani Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema licha ya baadhi ya wagombea wao kisiwani Pemba kuenguliwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Chama Cha Mapinduzi (CCM) hakitapata jimbo Pemba.

Maalim Seif aliyaeleza hayo juzi Mkoa wa Kaskazini Pemba katika Viwanja vya Jadida, Wete, katika mkutano wa hadhara ikiwa ni mwendelezo wa kampeni zake za urais.

Alisema atahakikisha majimbo ambayo wagombea wao wameenguliwa, wataelekeza wanachama wao kukipigia kura chama kingine na si CCM.

"Kama wao wanajifanya wanajua basi wajue na sisi tunajua zaidi na tutawaonyesha kuwa sisi ndio ACT- Wazalendo," alisema Maalim Seif.

Alisema CCM wasijipe tamaa kuwa watapata Jimbo la Pemba na kudai kuwa wananchi wa kisiwa hicho wamejipanga kuinyima CCM kura kama vipindi vilivyopita.

"Nakuombeni wanachama wetu mkae tayari tutakuelekezeni chama gani mkipigie kura, lakini si CCM," alisema.

Pia Maalim Seif aliwataka wafuasi wa chama hicho kisiwani Pemba kuichagua ACT-Wazalendo kuongoza Zanzibar ili wapate mamlaka kamili.

Maalim Seif aliwataka wafuasi hao kujitokeza katika uchaguzi mkuu ili waweze kutimiza malengo yao kwa kuipigia kura kwa wingi ACT -Wazalendo ili iongoze nchi.

"Vijana hii ni fursa ya mwisho kwetu lazima tukijikaze kuiondoa madarakani CCM ili tujitawale wenyewe," alisisitiza Maalim Seif. Alisema kutokana na Zanzibar kukosa mamlaka yake, imeshindwa kutekeleza miradi kwa kile alichokieleza mpaka wapate idhini Serikali ya Muungano.

"Mkinichaguwa nitaijenga Bandari ya Mpiga Duri Zanzibar bila hata kuiomba au kuiliza Serikali ya Muungano," alisema.

Sambamba na hilo alisema atajenga viwanja vya ndege vikubwa viwili Unguja na Pemba ili kuziwezesha ndege kubwa za kimataifa kutua katika viwanja hivyo. "Kwa sababu nimedhamiria kuwapatia wananchi ajira ni lazima nianzishe vyanzo vyangu vya kuwapatia ajira wote," alisema.

Katibu wa Habari, Uenezi na Mawasiliano ya Umma wa ACT -Wazalendo, Salim Bimani, aliitaka Jeshi la Polisi kuheshimu haki ya demokrasia na kuwataka wasifanyekazi kwa mihemko ya kisiasa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na watoto, Zunairah Abdalla Marzuk na Akla Abubakar Salum, walioandaliwa kwa ajili ya kumkabidhi mkasi wakati wa ufunguzi wa jengo jipya la Mama na Mtoto la Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja, juzi. **PICHA: IKULU**

# Mwanasheria ahoji usiri wa kura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWANASHERIA wa ACT-Wazalendo, Omar Said Shaban, amehoji kuwa ni kwa namna gani faragha na usiri wa kura ya mapema utalindwa wakati wa kuchanganya kura za mapema zitakazopigwa Oktoba 27 na zile za Oktoba 28.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho, Vuga Mjini Zanzibar.

Omar alisema chama hicho hakijaridhika na majibu ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kuhusu kura ya mapema kwa sababu bado yanaendelea kuacha maswali mengi na yameshindwa kutoa majibu hoja za msingi.

Alitaka ZEC kuweka wazi ikiwa mawakala wa vyama na wagombea wataruhusiwa kuwapo usiku wa kuamkia Oktoba 28 mahali ambapo masanduku ya kura yatahifadhiwa ambayo yana kura za mapema.

Pia alitaka ZEC kutoa ufafanuzi vipi usiri wa kura ya mpigakura utalindwa ikiwa bahasha ya kura ya mapema inaandikwa nambari ya kitambulisho cha mpigakura.

Naye Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, alisema kura ya mapema ni takwa la kikatiba na sheria, hivyo italindwa na mawakala wa vyama vya siasa wataruhusiwa kuwapo katika ulinzi wa kura hizo.

"Masanduku ya kura za mapema yatalindwa na vyombo vya ulinzi na usalama, lakini pia mawakala wa vyama vya siasa wataruhusiwa kuwapo kulinda kura hizo hadi Oktoba 28 ambayo ni siku ya wapigakura wote waliomo katika daftari," alisema Faina.

Aidha, mkurugenzi huyo alisema kuwa maandalizi ya uchaguzi yameshakamilika na Serikali ya Zanzibar imegharamia fedha zote bila ya kutegemea wafadhili.

"Huu ni uchaguzi pekee ambao serikali yenyewe imegharamia gharama zote za uchaguzi ambazo ni Sh. bilioni 9.1 zinazotokana na mapato yake ya ndani," alisema Faina.

# Dk. Mwinyi asema Muungano umeleta manufaa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Muungano wa Tanzania unawapa fursa Wazanzibari ya kuuza na kununua bidhaa zao kwenye soko kubwa zaidi la Tanzania Bara.

Alisema, Tanzania Bara kuna idadi kubwa ya watu ukilinganisha na Zanzibar kwa hivyo kama kuna bidhaa yoyote Zanzibar inayotaka kuuzwa, soko kubwa lipo Tanzania Bara.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo kwenye viwanja vya Mchanga Mdogo Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwa ni mwendelezo wa kampeni za urais za CCM.

"Sisi sote tunatambua kama kisiwa cha Zanzibar ni kidogo na kwamba si vitu vyote tunalima hapa kwa hivyo bidhaa nyingi tunategemea Tanzania Bara," alisema.

Mgombea huyo alisema isingekuwa Muungano, Zanzibar ingehitaji fedha nyingi za kigeni kununua vitu ambavyo vinanunuliwa sasa kutoka Zanzibar.

Alisisitiza kuwa kumekuwa na upotoshaji mkubwa kwamba kikwazo cha maendeleo ya Zanzibar ni Muungano na kusema jambo hilo ni kinyume chake na kwamba maendeleo ya Zanzibar yanatokana na Muungano uliopo.

Alisema anaamini kwamba Muungano wa Tanzania ni kielelezo tosha cha kuleta maendeleo ya haraka.

Pia aliwataka wananchi wa Zanzibar kutokuwa na mashaka na kwamba kuendelea kuwa na muungano huo ndio kutaweza kudumisha amani iliyopo.

Naye Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, alisema CCM inafanya mikutano yake miaka yote kwa ustaarabu.

Alisema hiyo ni tofauti na vyama vyengine vya kisiasa ambavyo hufanya mikutano yao kwa fujo bila ya kuzingatia amani ya nchi.

Pia alisema mara hii ushindi wa CCM kwa upande wa Pemba utakuwa wa mfano ambao haujawahi kutokea kwa miaka mingi.

Aliwaahidi wananchi wa Pemba na Wazanzibari wote kuwa usalama upo wa hali ya juu siku ya uchaguzi na kwamba wajitokeze kwa wingi kupiga kura bila ya kutishwa na mtu yeyote.

# Bilioni 13/- kutatua shida ya maji Geita

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAKAZI wa vijijini mkoani Geita wanatarajia kunufaika na huduma ya majisafi kutoka asilimia 60 hadi kufikia asilimia 75, ifikapo Desemba, 2020 baada ya Sh. bilioni 13 kupangwa kukamilisha miradi hiyo.

Meneja wa Wakala wa Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoa wa Geita, Mhandisi Nicas Ligombi alisema miradi hiyo ya maji utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali za ujenzi kati ya asilimia 70 mpaka asilimia 80 ili kukamilika.

"Hakika tunategemea ifikapo Desemba, 2020, kukamilisha miradi yote na kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika maeneo ya vijijini kwa Mkoa wa Geita kitaongezeka kutoka asilimia 60 hadi kufikia asilimia 75.

Mhandisi Nicas Ligombi alisema miradi hiyo yote ikikamilika maji yatakuwa yakipatikana kwa wingi na kuondoa tatizo la maji.

Naye Meneja wa RUWASA Wilaya ya Chato, Mhandisi Andrew Kilembe, alisema utekelezaji wa mradi wa maji wa Imalabupina Inchwankima umefika asilimia 90 katika ujenzi wa miundombinu ya maji na vijiji vitano kati ya 11 vinavyotakiwa kunufaika na mradi huo tayari vinapata huduma hiyo.

Vijiji vinavyopata huduma ya maji ni Nyamirembe, Kalebezo, Nyambiti, Busalala na Imalabupina Alisema mradi huo ukikamilika wananchi zaidi ya 59,000 watanufaika na huduma ya majisafi na salama katika vijiji vya Nyamirembe, Kalebezo, Nyambiti, Busalala Imalabupina, Inchwankima, Kachwamba, Ipandikilo, Idoselo, Mwangaza na Igalula .

Mhandisi Kilembe alisema hadi sasa mradi umefikia na asilimia 100 kwa upande wa ununuzi wa mabomba na fedha zilizokwishalipwa kwa makandarasi M. M. Industries na Ndeenengo Senguo Co. Ltd ni kiasi cha shilingi bilioni 7.2.

Wakati huo huo, Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Maji, Prosper Buchafwe, amewaelekeza watendaji hao wa RUWASA mkoani Geita kuongeza juhudi zaidi za usimamizi wa miradi ya maji ili wananchi wapate huduma hiyo mapema.




Baadhi ya wafanyabiashara wakitoa maji yaliyoingia kwenye maeneo yao ya biashara, eneo la Mwenge, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: FRANK MAXMILLIAN/TUDARCO**

# NEMC yazitaka halmashauri kuwavutia wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira nchini (NEMC) limeziomba halmashauri nchini kuweka mazingira safi na salama ili kulinda afya za watu na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

Mkurugenzi wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, ndiye aliyetoa wito huo, na kueleza kwamba mafanikio ya nchi ya kiuchumi lazima yaendane na ustawi, usimamizi na utunzwaji wa mazingira ili kulinda afya za watu, uhai wa viumbe wengine na kuwavutia wawekezaji.

"Nchi yetu imepata mafanikio makubwa. Ili mafanikio haya yawe endelevu, lazima halmashauri zihakikishe mazingira ni rafiki kwa jamii," alisema Dk. Gwamaka.

Dk. Gwamaka alisema mazingira yakiwa mazuri na salama, yatavutia wawekezaji wengi zaidi kutoka nje ya nchi, na mapato yataongezeka kutokana na kodi na hata kuchagiza fursa za ajira kwa vijana nchini.

"Natoa rai kwa halmashauri zetu kutambua kwamba hawa wawekezaji wanaangalia vitu vingi ikiwamo na mazingira ya eneo la kuwekeza, hivyo ni jukumu letu kushirikiana kwa pamoja kuweka maeneo yetu safi ili tuwavutie wawekezaji kuwekeza katika maeneo yetu," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema sasa ni wakati wa halmashauri kutambua fursa zilizomo kwenye taka, na kueleza kuwa taka zikichambuliwa vyema zinapata soko viwandani na kutoa mfano wa plastiki na chuma chakavu, ambayo amesema ni aina za taka ambazo hufanyiwa urejezwaji na kutumika kutengenezea bidhaa mpya.

"Tuache kuishi kimazoea. Halmashauri zetu zote ziwaongoze wananchi, na hasa vijana, wachangamkie fursa kwani taka kama vile chuma chakavu na plastiki ni aina ya taka zinazohitajika sana viwandani," alieleza Dk. Gwamaka.

Alitolea mfano Halmashauri ya Jiji la Mbeya na kusema imekuwa ikishirikiana kwa karibu sana na NEMC katika kutatua changamoto na matatizo ambayo yamekuwa yakiibuka mara kwa mara.

# Bosi RITA azuru Rukwa kukagua hali utendaji

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Kabidhi Wasii Mkuu, Emmy Hudson, jana alitembelea wilaya za Nkasi mkoani Rukwa, Mpanda na Tanganyika mkoani Katavi kwa lengo la kukagua maendeleo ya utendaji wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Bosi huyo wa RITA amezuru katika mikoa hiyo ili kujiridhisha kama utoaji wa huduma za usajili wa vizazi na vifo unazingatia na kufuata sheria na taratibu za usajili hususani katika maeneo hayo ya mipakani ambako kuna mwingiliano mkubwa wa wageni kutoka nchi jirani na utekelezaji wa utoaji huduma hizo kwa njia ya kielektroniki iliyoanzishwa mapema mwaka huu.

Akiwa katika ziara hiyo, Hudson alijionea utoaji wa huduma na kuzungumza na watumishi kuhusu kutanguliza uzalendo na uadilifu kwa ustawi na usalama wa taifa huku baadhi ya wananchi waliojitokeza kupatiwa huduma hizo wakisisitizwa kuhakikisha kila mmoja ndani ya familia au ukoo ahakikishe anasajiliwa na kupatiwa cheti cha kuzaliwa kutokana na umuhimu na uhitaji wakati wa kupatiwa baadhi ya huduma za msingi.

Alisema huduma hizo ni pamoja na vitambulisho vya taifa, hati za kusafiria, matibabu ya bima ya afya, elimu ya msingi na sekondari na mikopo kwa wanafunzi wanaoomba kujiunga na elimu ya juu.

Katika ziara yake mkoani Katavi, kiongozi huyo aliwataka wananchi kutumia huduma za usajili wa vizazi na vifo kwa njia ya kielekroniki iliyoanzishwa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma hizo kwa wakati.

Hudson alisisitiza kuwa, lengo la kuanzisha kutoa huduma kwa njia ya kielekroniki ni kumpatia fursa mwananchi wakati akiendelea na shughuli nyingine za ujenzi wa taifa huku akipatiwa huduma kule anakoishi ili kurahisisha muda na gharama za usafiri wakati wa kufuatilia huduma hizo.

"Kwa sasa mwananchi anaweza kuomba cheti cha kuzaliwa au kifo akiwa nyumbani kwake na kuonyesha sehemu ambayo angependa kuchukulia cheti hicho," alisema Hudson.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Sostenes Mayoka, alisema kwa sasa wamejipanga kuwahudumia wananchi licha ya vikwazo kadhaa vilivyopo vikiwamo vya wahamiaji haramu, huku akisisitiza watu wasisubiri matukio au vyeti vihitajike ndiyo wafuatilie vyeti vya kuzaliwa.

"Kwa sasa umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa umeongezeka ambapo watoto wanaojiunga na elimu ya msingi au sekondari wanatakiwa kuwa na vyeti vya kuzaliwa, hati ya kusafiria, vitambulisho vya taifa pamoja na bima ya afya, kuvipata lazima uwe na cheti hicho," alisema.

HABARI KIMATAIFA

## Rwanda yahalalisha mauzo ya bangi nje

**KIGALI,** Rwanda

NCHI ya Rwanda imehalalisha kisheria ukulima na mauzo ya nje ya nchi ya mmea wa bangi kwa ajili ya matumizi ya tiba ili kupata fedha.

Kikao cha Baraza la Mawaziri kilichokaa Jumatatu kiliidhinisha miongozo kuhusu ukulima, usindikaji na mauzo ya nje ya mimea ya matibabu ya thamani ya juu nchini Rwanda. Akizungumza na televisheni ya taifa, jana Waziri wa Afya nchini humo, Dk. Daniel Ngamije, alisema mimea hiyo inajumuisha bangi.

Taifa hilo lililopo Afrika Mashariki limehalalisha bangi baada ya nchi ya Malawi, Lesotho, Afrika Kusini, Zambia na Zimbabwe kufanya hivyo.

Ngamije alisema Rwanda inataka kutoa mchango wake kwa vituo vya utafiti na sekta ya dawa kwa kutoa rasilimali ili wapate faida ya fedha.

Mwaka jana, soko la bangi la dunia lilidhaniwa kuwa na thamani ya dola bilioni 150, kulingana na Benki ya Barclays.

"Ni wakulima waliopewa leseni ambao wataruhusiwa kuzalisha zao hili, uvutaji wa bangi bado unazuiwa," hiyo ni kulingana na Bodi ya Maendeleo ya Rwanda.

Iwapo utapatikana unalima au kuuza bangi nchini Rwanda unaweza kuadhibiwa hadi kifungo cha maisha jela, huku mvutaji akikabiliwa na kifungo cha miaka miwili jela. **BBC**

## Ofisi ya Bobi Wine yavamiwa

**KAMPALA,** Uganda

OFISI ya chama cha mgombea urais nchini Uganda, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi imevamiwa na wanajeshi wenye silaha pamoja na maofisa wa polisi.

Nyaraka zimeripotiwa kuchukuliwa kutoka kwenye ofisi hiyo pamoja na kofia yenye muundo wa kijeshi na kamera za CCTV.

Mmoja wa washauri wa Bobi ameiambia BBC kuwa maofisa hao hawakuwasilisha kibali walipokuwa wakiingia kukusanya nyaraka na mavazi hayo.

Msemaji wa Polisi nchini Uganda, Fred Enanga, ameiambia BBC kuwa, wanafanya operesheni kuhusu utumiaji mbaya wa sare za kijeshi.

Mwezi Septemba, mwaka jana serikali iliidhinisha kofia nyekundu sawa na anayovaa Bobi Wine na wafuasi wake kuwa ni sare ya jeshi ikimaanisha yeyote anayeonekana ameimiliki au kuivaa kinyume cha sheria anaweza kushtakiwa.

Enanga alisema operesheni inaendelea na kwamba maofisa watasaka maeneo mengine pamoja na ofisi za National Unity.

Bobi Wine alisema kuwa nguvu za dola zinamlenga na chama chake wakati akijiandaa kukabiliana na Rais Yoweri Museveni katika uchaguzi ujao wa mwakani.

Lakini msemaji wa polisi anasisitiza kuwa operesheni hiyo haijachochewa kisiasa. **BBC**

# WB yatoa mabilioni chanjo dhidi ya corona

**WASHINGTON,** Marekani

BENKI ya Dunia (WB) imeidhinisha kiasi cha Dola za Marekani bilioni 12 kwa ajili ya chanjo ya virusi vya corona kwa nchi zinazoendelea ili kugharamia ununuzi, usambazaji, vipimo na matibabu.

Taarifa iliyotolewa na benki hiyo juzi ilisema fedha hizo ni sehemu ya mpango wa jumla wa msaada wa dola bilioni 160 utakaotolewa hadi katikati ya mwaka 2021, ili kuzisaidia nchi hizo kukabiliana na janga hilo.

**Fedha hizo ni sehemu ya mpango wa jumla wa msaada wa dola bilioni 160.**

Msaada huo wa kifedha utakaowanufaisha karibu watu bilioni moja, utafadhili utafiti kwa kampuni za utengenezaji dawa pamoja na kuratibu matayarisho ya kupokea na kusambaza chanjo za corona kwenye mataifa yanayoendelea.

Ingawa bado hakuna chanjo ya corona, WB ilisema ni muhimu kwa mataifa hayo kujiweka tayari kwa sababu usambazaji wa chanjo ni mchakato wenye vikwazo visivyotabirika. **DW**



Kikosi maalumu cha kupambana na wizi nchini Nigeria kinachoshutumiwa kwa ukatili. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Bomu la vita ya pili ya dunia lalipuka

**WARSAW,** Poland

BOMU kubwa ambalo halikulipuka katika vita ya pili ya dunia lililobainika nchini Poland limelipuka wakati wa shughuli ya kulitegua.

Msemaji wa Jeshi la Wanamaji nchini humo aliyasema hayo jana.

Uwezekano wa bomu hilo lililokuwa chini ya bahari kulipuka ulikuwa ukitarajiwa na wapiga mbizi wote waliohusika kwenye tukio hilo.

Karibu wakazi 750 waliondolewa mji wa bandari wa Swinoujscie.

Bomu hilo liitwalo Tallboy au 'tetemeko la ardhi' lilidondoshwa wakati wa vita ya pili ya dunia na kuizamisha meli ya Ujerumani Lützow.

Swinoujscie ilikuwa sehemu ya Ujerumani na kuiita Swinemünde wakati wa ulipuaji.

Mtikisiko wakati wa kulitegua bomu hilo ulisikika katika sehemu za mji na video zinaonesha mlipuko mkubwa na maji mengi yakiruka angani.

Bomu hilo lilikuwa na urefu wa mita 6 na uzito wa tani 5.4, karibu nusu ya bomu hilo liliundwa na vilipuzi.

Lilikuwa limetua kwenye kina cha mita 12 na sehemu ya pua ya bomu hilo ilikuwa ikichungulia nje.

Jeshi la Wanamaji walitumia chombo kilichokuwa kikidhibitiwa kutoka mbali kwa ajili ya kujaribu kuchoma bomu hilo, mbinu ambayo kama ikifanikiwa kuchoma mifumo ya chaji za vilipuzi bila kusababisha mlipuko, mwanahabari wa BBC Adam Easton anaripoti kutoka Warsaw.

"Mbinu hiyo ya kuchoma iligeuka mlipuko. Chombo hicho kimeelezwa kuwa kimepozwa, hakitasababisha tishio lolote tena kwa njia za meli za Szczecin-Swinoujscie.

"Wapigambizi wote walitoka katika eneo la hatari wakiwa salama," alisema Luteni Kamanda Grzegorz Lewandowski ambaye ni msemaji wa jeshi la maji wa gadi ya nane ya ulinzi wa pwani Flotilla. **BBC**

## Wanasayansi wameonya mlipuko wa volcano DRC

**KINSHASA,** DRC

WANASAYANSI wameonya kuwa Ziwa la Lava linajaa juu kwa kiwango cha kutisha katika Mlima wa Volcano wa Nyiragongo uliopo mji wa Goma Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mwezi Januari 2002, lava ilimwagika kutoka Mlima Nyiragongo kwa kasi hadi katika mji wa Goma na kusababisha vifo vya watu 250 na kuharibu asilimia 20 ya mji wa Goma.

Kikundi cha wanasayansi wanaochunguza matukio ya milima, wameonya kuwa, mwamba unaoyeyuka unaweza kulipuka tena kupitia kuta za ziwa la volcano.

"Hali inaonyesha dalili za mkasa mwingine," Dario Tedesco, mtaalamu wa volcano na milima aliliambia jarida la masuala ya kisayansi. **BBC**

# KANTE ATIBUANA NA LAMPARD CHELSEA




**LONDON,** England

NI wazi kwamba, muda wa kiungo Chelsea, N'golo Kante kuendelea kucheza pale Stamford Bridge unaelekea mwisho.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Kante na kocha wake, Frank Lampard wameingia kwenye bifu ambalo litamfanya nyota huyo kuamua kuondoka klabuni hapo.

Licha ya kutompa nafasi ya kuanza mara kwa mara, Kante anaweza kuondoka ndani ya timu hiyo Januari baada ya kuzozana na Lampard.

Kwa mujibu wa ripoti, Lampard alikataa kumpa ruhusa ya kwenda kwenye sherehe ya ndoa ya rafikiye.

Kiungo huyo ambaye ni miongoni mwa wanaofanya vizuri duniani kwa sasa na ndani ya timu yake ya Taifa ya Ufaransa kwa sasa yupo kwenye majukumu yake ya timu ya taifa.

Ripoti zinaeleza kuwa Lampard aligomea ishu ya Kante kuacha mazoezi kwa muda na kuhudhuria sherehe ya harusi ya rafikiye kabla ya mapumziko mafupi yaliyotokana na timu za taifa kuwa kwenye majukumu.

# Keane apewa timu England

**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa zamani wa Manchester United, Roy Keane, anatarajiwa kuchukua mikoba ya kuinoa timu ya Salford ya Daraja la Pili nchini England.

Timu hiyo ya Salford inamilikiwa na kundi la wachezaji wa zamani wa Man United ambao ni marafiki maarufu kama "Class of 92" ambao ni Gary Neville, Phil Neville, Ryan Giggs, David Beckham, Paul Scholes na Nicky Butt.

Mabosi hao wamemfuta kazi kocha Graham Alexander, Jumatatu wiki hii na wanafikiria kumpa kazi ya kukinoa kikosi hicho Keane.

Hata hivyo, wakati mchakato wa kumpa Keane kibarua hicho ukianza, kwa sasa Scholes atakuwa kocha wa muda kuendeleza jahazi la kuwania nafasi ya kupanda hadi Championship msimu ujao.

Kwa sasa Salford iko nafasi ya tano kwenye msimamo ikishinda mechi tatu na kutoka sare mara mbili katika mechi tano ilizocheza mpaka sasa.

Keane akiwa ameongozana na Neville na Scholes alikuwapo kutazama mchezo wa Salford dhidi ya Tranmere ulioisha kwa sare ya mabao 2-2 ukiwa ndio wa mwisho kwa Alexander akiwa kocha kabla ya kufutwa kazi.

Kwa mujibu wa The Mirror, Keane anajiandaa kurejea kwenye kazi ya ukocha tangu alipoamua kujiweka kando mwaka 2018 wakati huo akiwa kocha msaidizi kwenye timu ya Taifa ya Ireland chini ya Martin O'Neill.

Kwa sasa Keane ni mchambuzi wa Sky Sports akiwa amepata kuzinoa Sunderland, Ipswich, Aston Villa na Nottingham Forest.







# *Martinez aisifia Argentina kuvunja mwiko kwa Bolivia*

**LA PAZ,** Bolvia

LAUTARO Martinez amesifia kiwango cha Argentina wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Bolivia kwenye mechi ya kufuzu kucheza Kombe la Dunia, juzi Jumanne.

Joaquin Correa alifunga bao la ushindi la dakika ya 79 kwa kikosi hicho cha kocha, Lionel Scaloni, ambapo sasa kimeibuka na ushindi wa mechi zote mbili za kufuzu.

Huo ulikuwa ni ushindi wa kwanza kwa Argentina kwa Bolivia tangu mwaka 2005 wakati wakipata pointi zote tatu muhimu hapa La Paz.

Martinez, alifunga bao la kusawazisha lile la Marcelo Martins Moreno, ambalo lilikuwa la ufunguzi kwa Bolivia.

"Tulijua kwamba mchezo ungekuwa mgumu sana, lakini nafikiri timu yetu ilikuwa kwenye kiwango bora zaidi," alisema mshambuliaji huyo wa Inter baada ya mchezo huo.

"Tuna furaha kubwa."

Martinez aliongeza: "Tulikuwa na wakati mgumu, kwani wapinzani wetu walikuwa bora na tulitakiwa kupambana sana.

"Hata historia inaonyesha kwamba, Bolivia wanakuwa wagumu sana kwetu, lakini kwa hakika nina amani na ushindi huu."

# Janga la corona lamkumba Ronaldo

**LISBON,** Ureno

NYOTA wa timu ya Taifa ya Ureno na Klabu ya Juventus, Cristiano Ronaldo, atalazimika kujitenga baada ya kugundulika na virusi vya corona, Shirikisho la Soka nchini la Ureno (FPF), limethibitisha.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 35, anaendelea vizuri bila dalili huku akijitenga mwenyewe kwa angalau siku 10, taarifa ya FPF imethibitisha.

Jana Jumatano timu ya Taifa ya Ureno ilicheza na Sweden katika mchezo wa Ligi ya Mataifa UEFA na Ronaldo akaukosa mchezo huo.

Wachezaji wengine wote wamesalimika baada ya kupimwa hivyo kuendelea na majukumu yao.

Ronaldo alikuwa sehemu ya kikosi wakati Ureno inatoka sare tasa na Ufaransa mchezo uliopigwa Ufaransa Jumapili.

Mchezaji huyo ambaye ni nahodha wa kikosi hicho, aliandikisha rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufikisha mabao 100 ngazi ya timu ya taifa.

Kutokana na matokeo ya kujitenga, kuna uwezekano mkubwa Ronaldo akakosa mechi za klabu yake ya Juventus kwenye Ligi Kuu ya Italia, Seria A, dhidi ya Verona na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Dynamo Kiev, Oktoba 20.



# RAMOS AWINDWA JUVE, PSG



**TURIN,** Italia

SERGIO Ramos ameripotiwa kwamba anaondoka Real Madrid na kwenda ama Juventus au Paris Saint-Germain.

Nahodha huyo wa Madrid, Ramos mwenye umri wa miaka 34, amekuwa akicheza pale LaLiga tangu mwaka 2005, lakini mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Na sasa miamba ya Ulaya wamekuwa wakimkodolea macho, kwani bado hajaongeza mkataba na miamba hao wa dimba la Santiago Barnabeu.

Juventus na PSG zinaonekana kuwa mstari wa mbele kumnyatia nyota huyo wa Madrid, kwa mujibu wa gazeti la El Chiringuito.

Mkataba wa Ramos unamalizika Juni mwakani, na hivyo sasa uvumi juu ya majaliwa yake umeanza kuibuliwa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, ameshinda mataji matano ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Madrid.

# *Griezmann mambo magumu Ufaransa*

**PARIS,** Ufaransa

DIDIER Deschamps amesema hawezi kumwahidi Antoine Griezmann kuwa na nafasi kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa hata kama takwimu zake kwenye timu hiyo kuwa za kuvutia.

Griezmann amekuwa na wakati mgumu wa kuwa kwenye ubora wake tangu alipohamia Barcelona akitokea Atletico Madrid Julai mwaka 2019, kwa klabu na timu ya taifa.

Alikuwa mchezaji bora wa michuano ya Euro 2016, na pia akashinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa miaka miwili iliyopita, lakini katika umri wake wa miaka 29 sasa, anaonekana kutokuwa kwenye kiwango chake.

Deschamps anaamini anaweza kurudi kwenye kiwango chake na kusema hana shaka kabisa na Griezmann.

Lakini kocha huyo amebainisha kwamba, ni vigumu kumhakikishia nafasi kwenye kikosi hicho.

"Najua kwamba ana takwimu nzuri kwenye kikosi hiki, na zinaongea wazi kwamba amecheza mechi 81 mabao 32 na pasi za mwisho 21. "Takwimu hizi zinazungumza wazi kabisa. Lakini siwezi kumwahidi chochote kama ilivyo kwa wachezaji wengine."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR ASIFIWA KUVUNJA REKODI YA RONALDO BRAZIL

●●● Kila wakati una historia yake, katika kila kizazi kina rekodi zake kulikuwa na Rivaldo...

**SAO PAULO,** Brazil

KOCHA Mkuu wa Brazil, Tite amemsifia Neymar na kusema nyota huyo amekuwa bora zaidi baada ya kuipiku rekodi ya Ronaldo kwenye orodha ya wafungaji bora wa nchi hiyo.

**Neymar mwenye umri wa miaka 28, alifunga mabao matatu 'hat-trick' wakati Brazil ilipopata ushindi wa 4-2 dhidi ya Peru kwenye kufuzu Kombe la Dunia juzi Jumanne.**

Akiwa na mabao 64, amempiku Ronaldo mwenye mabao 62, huku akiwa amepitwa na Pele pekee mwenye mabao 77.

Tite alimsifia sana Neymar, ambaye alifunga kwa penalti mbili katika ushindi huo ambapo Peru walimaliza wakiwa na wachezaji 10 uwanjani.

"Kila wakati una historia yake, katika kila kizazi kina rekodi zake," alisema Tite baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Alikuwa Ronaldo, kulikuwa na Rivaldo, Romario, Bebeto, kila mmoja kwa wakati wake.

"Si haki kuwalinganisha hawa, kwani kila mmoja na wakati wake na rekodi yake kwenye kikosi cha Brazil.

"Ninachoweza kusema sasa ni kwamba, Neymar ameweka rekodi yake katika wakati wake. Kwa sasa yeye ndiye mchezaji muhimu kwa Brazil. "Ni mchezaji anayefunga na kusaidia kupatikana mabao na mmaliziaji mzuri sana, anazidi kuwa bora na bora zaidi huku akizidi kupevuka."

Brazil walikuwa nyuma mara mbili dhidi ya Peru wakati Andre Carrillo na Renato Tapia walipofunga, na mabao hayo yakasawazishwa na Neymar na Richarlison.

Kucheza dhidi ya Peru mara zote ni mchezo mgumu. Wana kikosi kizuri na imara, lakini tulikuwa vizuri na tukaondoka na ushindi," alisema Tite.

## ZISIKUPITE

### BARCA KWA POGBA, ALABA

BARCELONA wanajiandaa kuwanasa nyota wawili, Paul Pogba mwenye umri miaka 27, na kiungo wa Bayern Munich na Austria, David Alaba, 28. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### LEEDS KWA NYOTA ENGLAND

LEEDS United wanamwania kiungo wa Norwich City na timu ya England chini ya miaka 21, Todd Cantwell mwenye umri wa miaka 22, pamoja na kiungo wa Derby County na England chini ya miaka 19, Louie Sibley mwenye miaka 19. ***(Yorkshire Evening Post)***

### DILI LA BENRAHMA LIMEIVA

KLABU ya West Ham na Brentford zimekubaliana kuhusu uhamisho wa pauni milioni 30 wa mshambuliaji, Said Benrahma mwenye umri wa 25, lakini bado hawajafikia makubaliano ya maslahi binafsi na mshambuliaji huyo wa Algeria. ***(Sky Sports)***

### ROSE HUYOOO MIDDLESBROUGH

KLABU ya Middlesbrough imeweka mkakati wa kumnasa mlinzi wa kushoto wa England na Tottenham, Danny Rose mwenye umri wa 30. ***(Football Insider)***

### ROMERO KUACHANA NA UNITED

GOLIKIPA wa Manchester United, Sergio Romero, mwenye umri wa miaka 33, anataka kuvunja mkataba mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi huu, akitaka kuhamia Ligi ya Marekani. ***(Sun)***

### PALACE KUMSAKA CLYNE

KLABU ya Crystal Palace inakaribia kukamilisha uhamisho wa mkataba mfupi wa beki wa kulia, Nathaniel Clyne mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni mchezaji huru kwa sasa baada ya kuondoka Liverpool kipindi cha majira ya joto. ***(The Athletic)***

### WILSON SASA AGOMBEWA

TIMU za Cardiff na Swansea zinapambana kuwania saini ya kiungo wa Liverpool na Wales, Harry Wilson, 23, kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Wales Online)***

### POGBA AUNGWA MKONO UTD

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, anaendelea kuungwa mkono na wenzake ndani ya Manchester United licha ya kueleza shauku yake ya kuichezea klabu ya Real Madrid. ***(Manchester Evening News)***

### KEAN AFURAHIA MAISHA PSG

STRAIKA wa Everton na Italia, Moise Kean mwenye umri wa miaka 20, amebainisha hajutii kuondoka soka la Uingereza na kwenda Paris St-Germain. ***(Mail on Sunday)***

### MATA AWAKATALIA WAARABU

KIUNGO wa Manchester United na Hispania, Juan Mata, 32, alikataa ofa ya mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki kutoka timu ya Saudi Arabia. ***(Sport)***

### BALOTELLI APATA TIMU

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Italia na timu za Manchester City na Liverpool, Mario Balotelli, 30, ambaye yuko huru sasa baada ya kuondoka Brescia, atasajiliwa na klabu mpya ndani ya wiki chache zijazo. ***(Goal)***

# HABARI MICHEZO

## Mayanja aomba kuinoa Ihefu FC

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Simba, Mganda Jackson Mayanja (pichani chini) ni miongoni mwa makocha waliomba kazi ya kukinoa kikosi cha Ihefu FC, kilichoingia sokoni kutafuta mrithi wa kuchukuwa nafasi ya Maka Mwalwisi aliyetimuliwa.

Hivi karibuni uongozi wa Ihefu ulimfuta kazi kocha wao, Mwalwisi kutokana na mwenendo mbovu wa matokeo ya timu yao hiyo katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Ihefu FC, Fred Chalamila, alisema kuna makocha wengi ambao wametuma wasifu wao (CV) kuomba kazi akiwamo Mayanja ambaye aliwahi kuwa Kocha Msaidizi wa Simba chini ya Mcameroon Joseph Omog.

Alisema kocha mwingine ni Hermana Haruna aliyewahi kuwa kocha mkuu wa KMC FC.

"Makocha hao ni baadhi ya walimu waliotuma CV kwangu, kuna wengine ambao wametuma kwa mmiliki, kiufupi mchakato unaendelea kutafuta kocha mkuu," alisema Chalamila.



Alisema bado wanaendelea kupokea CV za makocha mbalimbali ikiwamo ndani na nje ya nchini, baada ya hapo bodi ya wakurugenzi itakutana na kuangalia nani ambaye anastahili kupewa jukumu la kuwa kocha mkuu wa timu hiyo iliyoshinda mchezo mmoja tu kati ya mitano iliyocheza kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Biashara United.

Ihefu ambayo jana ilikuwa ugenini dhidi ya Biashara United ya Mara, inashika nafasi ya pili kutoka mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo ambayo kinara ni Azam FC ikiongoza kwa kuvuna pointi zote 15 katika mechi tano ilizocheza, huku Mbeya City ikiburuza mkia ikiwa na lama moja tu.

Lakini pia baada ya JKT Tanzania iliyoruhusu nyavu zake kutikiswa mara nane, Ihefu na Mbeya City ndizo timu zinazofuata kwa kuruhusu kufungwa mabao mengi (saba) hadi ligi hiyo inafikia raundi ya tano kabla ya mzunguko wa sita kuendelea jana.

Ushindi pekee kwa Ihefu msimu huu, iliupata nyumbani katika Uwanja wa Sokoine dhidi ya Ruvu Shooting, kwa kushinda bao 1-0.

# AZAM, MWADUI ZAIDI YA VITA CHAMAZI LEO

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC, leo wanashuka tena dimbani baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa za Kalenda ya FIFA, kusaka pointi tatu dhidi ya Mwadui FC kwenye mechi itakayopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam majira ya saa 1:00 usiku.

**Ni mechi itakayokuwa inafuatiliwa na mashabiki wengi wa soka nchini, wakiwa na lengo la kuona kama Azam itakuwa na mwendelezo wao mzuri wa kushinda kwa asilimia 100, ambao wameuonyesha mpaka sasa.**

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, amesema maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na hakuna majeruhi yeyote kwenye kikosi chao.

"Hatuna majeruhi, tumejipanga vizuri na hivi sasa tunawasubiri wachezaji wengine, Yakubu Mohamed na Nicolaus Wadada ambao walikuwa kwenye majukumu yao kwenye timu zao za taifa," alisema Zacharia.

Tayari Azam FC imeshacheza mechi tano, ikishinda zote wakati huu ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu, ikiwa na pointi 15 na mabao ya kufunga tisa, ikifungwa mawili pekee.

Ilianza ligi kwa kuifunga Polisi Tanzania bao 1-0, Coastal Union mabao 2-0, Mbeya City 1-0, Prisons 1-0, na Kagera Sugar 4-2.

Azam kama kawaida itaundwa na safu yake ya ushambuliaji ikiongozwa na Mzimbabwe Prince Dube ambao ndiye kinara wa ufungaji mabao mpaka sasa kwenye ligi akiwa ameshapachika mabao matano, na Mzambia Obrey Chirwa mwenye mabao mawili mpaka sasa, huku kwenye ulinzi kukiwa na mchezaji wa timu ya Taifa ya Ghana, Yakubu na golini huenda akakaa yule yule David Kissu, ambaye kwa sasa anaunyemelea 'U-Tanzania One' langoni.'

Kwa upande wa Mwadui inabidi iingie kwa tahadhari kwenye Uwanja wa Azam Complex, kwani hakuna timu iliyoingia hapo ikapona msimu huu.

Kocha Mkuu wa Mwadui Khalid Adam, amesema Azam isitarajie mechi nyepesi kwa sababu ana uzoefu wa kuzifunga timu ambazo hazijapoteza mechi.

"Timu iko vizuri, na najua nakwenda kucheza kwenye uwanja ambao Azam haijapoteza na wao hawajapoteza mechi, lakini hata Simba msimu uliopita walikuwa hawajapoteza mechi tukawa wa kwanza kuwafunga. Lakini kumbuka pia kuwa na sisi tumetoka kushinda ugenini dhidi ya Namungo, kwa hiyo tutapambana," alisema kocha huyo.

Katika mechi ya mwisho ya raundi ya tano, Mwadui ikiwa ugenini ilishinda bao 1-0 dhidi ya Namungo FC.

Timu hiyo inakamata nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi sita, ikishinda mbili na kufungwa tatu.

## KATUSUA...




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Elia Nzinza, kutoka Kibaha mkoani Pwani, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. 10,619,725 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya mechi za mpira wa miguu wiki iliyopita. Jackpot ya SportPesa wiki hii imefikia Sh. 235,834,940. **PICHA: SPORTPES**

## *Makalani kuvaa viatu vya Nonga wakiialika Mtibwa*

**Saada Akida**

MSHAMBAULIAJI wa Gwambina FC, Paul Nonga, leo ataikosa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar, utakaopigwa katika Uwanjani wao uliopo Misugwi, Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Gwambina, Fulgence Novatus, alisema kukosekana kwa nyota huyo haitaathiri mipango yake kwani amemwandaa Japhet Makalani kuchukuwa nafasi hiyo.

Alisema amefanya maandalizi mazuri na kikosi chake tayari kwa kupambana kutafuta pointi tatu katika mechi hiyo watakayocheza katika uwanja wao wa nyumbani.

"Tumejipanga vizuri, kikosi kipo fiti bali nitamkosa Nonga aliyetonesha jeraha alilokuwa nalo katika mechi dhidi ya Ihefu, nafasi yake atacheza Makalani amerejea baada ya kutoka katika majeruhi na sasa yupo fiti kupambana tunataka pointi muhimu katika mechi yetu hiyo," alisema Fulgence.

Alisema itakuwa mechi ya ushindani kwa sababu wapinzani wao wamepoteza michezo miwili, hali ambayo anaamini nyota wake wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanalipa pointi katika uwanja wa nyumbani.

"Tuna waheshimu Mtibwa ni timu nzuri na watakuwa wamejipanga kuja kutafuta pointi, itakuwa mechi ya ushindani mkubwa kwetu na kwao pia," alisema Fulgence.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuber Katwila, alisema mikakati yake ni kuona kikosi chake kinapambana kutafuta pointi tatu za ugenini katika mechi yao dhidi ya Gwambina.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 15, 2020

Nipashe



Ramos awindwa Juventus, PSG

UKURASA 21

HAT-TRICK...



Straika wa Brazil, Neymar akishangilia baada ya kukwamisha mpira nyavuni katika moja kati ya mabao matatu (hat-trick) aliyofunga wakati wakiibuka na ushindi wa 4-2 dhidi ya Peru kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Amerika Kusini iliyopigwa Uwanja wa Taifa wa Lima, Brazil usiku wa kuamkia jana. **PICHA: HABARI UK. 22**

# DUBE AKIPOTEZEA KIATU CHA KAGERE

## ●●● Alia viwanja vya ugenini ni changamoto kwake kuweza kuhimili mbio hizo na kwamba...

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU akitajwa kuwa miongoni mwa washambuliaji wanaoweza 'kumvua' Kiatu cha Ufungaji Bora' Ligi Kuu Bara, straika wa Simba, Mnyarwanda Meddie Kagere, mshambuliaji wa Azam FC, Mzimbabwe Prince Dube, amesema changamoto ya ubovu wa viwanja vya ugenini ni moja ya sababu ya kizuizi kwake kuweza kufikia malengo yake.

**Hadi sasa wakati leo Azam ikitarajiwa kushuka dimbani dhidi ya Mwadui FC kwenye mechi yao ya raundi ya sita ya ligi hiyo, Dube yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji bora akiwa na mabao matano moja mbele ya Kagere anayefuatiwa na mchezaji mwenza wa Simba, Mkongomani Chris Mugalu aliyecheka na nyavu mara tatu.**

Lakini Dude ambaye atakuwa na nafasi ya kuendeleza mbio hizo za kumnyang'anya Kagere kiatu hicho alichokitwaa msimu uliopita kwa mara ya pili mfululizo baada ya kuhitimisha ligi hiyo akiwa na mabao 22, amesema anapata tabu sana ya kucheza soka lake anapokuwa nje ya Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na mwandishi wetu, Dube alisema mara nyingi anapocheza mechi za ugenini anatumia nguvu nyingi, na inamlazimu kucheza mipira ya juu kutokana na ubovu wa viwanja tofauti na wanapokuwa dimba lao la nyumbani ambapo pasi nyingi humfikia vizuri kutokana na ubora wa Uwanja wa Azam Complex.

"Viwanja vya ugenini haviko vizuri, mara nyingi ninapokuwa ninacheza ugenini huwa sifurahii kabisa mpira, na ninapata tabu kufunga kutokana na hali hiyo," alisema Dube.

Alisema hawazii kuwa mfungaji bora kwa kuwa bado ni mapema, hajazoea viwanja vya ugenini na ligi inaendelea, ila kwa sasa anachokiangalia ni kufanya vizuri kwenye mechezo iliyopo mbele yao kwa maslahi ya timu.

Katika mabao matano aliyofunga Dube hadi sasa, moja tu ndilo alilofunga uwanja wa ugenini wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

Wakati Kagere ambaye tayari ana uzoefu na viwanja vya ugenini hapa nchini, yeye amefunga mabao mawili sawa na aliyofunga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa unaotumiwa na Simba kama wa nyumbani.

Mabao mawili ya ugenini kwa Kagere, alifunga katika mechi dhidi ya JKT Tanzania wakati Simba ikishinda 4-0 kwenye mchezo wa raundi ya tano uliyopigwa Uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma, kabla ya timu kwenda mapumziko kupisha mechi za kimataifa zilizopo kwenye Kalenda ya Fifa.

Akizungumzia mchezo wao wa leo dhidi ya Mwadui ambao utachezwa kwenye uwanja anaoufurahia wa Azam Complex, Dube alisema anatambua utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kwa kuwa kila timu inahitaji matokeo lakini wapinzani wao ni wazuri.

Alisema Mwadui ni timu nzuri ambayo wachezaji wake wanacheza kitimu kwa ukishirikiano mkuwa lakini huonyesha nidhamu mchezoni.

"Niliiona timu hiyo namna inavyocheza wakati ikicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Azam Complex na kufungwa bao1-0, wanacheza vizuri kwa ushirikiano," alisema.

Alisema kikubwa kwake ni kuhakikisha anashirikiana na wachezaji wenzake kufunga mabao na kutoka na pointi tatu uwanjani, lakini akiwaomba mashabiki wa Azam kuendelea kuwapa sapoti kama walivyofanya katika michezo iliyopita.

Kama ambavyo Dude alivyo kileleni mwa orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Bara, ndivyo ilivyo pia kwa timu yake ambayo hadi sasa inaongoza mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo ikiwa na pointi 15 baada ya kushinda mechi zote tano ilizocheza.

## Griezmann mambo magumu Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

DIDIER Deschamps amesema hawezi kumwahidi Antoine Griezmann kuwa na nafasi kwenye kikosi cha timu ya Taifa...



HABARI UK 21

## Azam, Mwadui zaidi ya vita leo

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC, leo wanashuka tena dimbani baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa...



HABARI UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002